JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE), 2022

# KISWAHILI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE), 2022

# 121 KISWAHILI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2022**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO


DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI ........ 2

2.1 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA ........ 2

2.1.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ........ 2

2.1.1.1 Swali la 1: Ufahamu ........ 2

2.1.1.2 Swali la 2: Utumizi wa Lugha ........ 8

2.1.1.3 Swali la 3: Utumizi wa Lugha ........ 12

2.1.1.4 Swali la 4: Matumizi ya Sarufi ........ 17

2.1.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAREFU ........ 20

2.1.2.1 Swali la 5: Uandishi wa Barua Rasmi ........ 20

2.1.2.2 Swali la 6: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili ........ 24

2.1.2.3 Swali la 7: Asili ya Kiswahili ........ 29

2.1.2.4 Swali la 8: Tafsiri na Ukalimani ........ 35

2.2 SEHEMU YA II: KISWAHILI KARATASI YA PILI ........ 43

2.2.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ........ 43

2.2.1.1 Swali la 1: Fasihi kwa Ujumla ........ 43

2.2.1.2 Swali la 2: Maendeleo ya Fasihi Simulizi ........ 48

2.2.1.3 Swali la 3: Maendeleo ya Fasihi Simulizi ........ 52

2.2.1.4 Swali la 4: Usanifu wa Maandishi ........ 56

2.2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAREFU ........ 61

2.2.2.1 Swali la 5: Uhakiki wa Ushairi ........ 61

2.2.2.2 Swali la 6: Uhakiki wa Ushairi ........ 67

2.2.2.3 Swali la 7: Uhakiki wa Riwaya ........ 74

2.2.2.4 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya ........ 81

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA ........ 87

4.0 HITIMISHO ........ 88

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ........ 88

Kiambatisho A ........ 90

Kiambatisho B ........ 91

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa kuhusu uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa Kidato cha Sita mwaka 2022 kwenye somo la Kiswahili. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanafunzi, walimu, wazazi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla.

Taarifa hii inalenga kutathmini muhtasari wa Kidato cha Tano hadi cha Sita ili kuonesha mafanikio ya mfumo wa elimu kwa ujumla, hususani katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kimsingi tathmini ya majibu ya watahiniwa katika mtihani huu inalenga kuonesha dhahiri yale ambayo mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa katika elimu ya sekondari kwa Kidato cha Sita.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu kwa mwaka 2022 zinaonesha kuwa, watahiniwa 24,944 sawa na asilimia 100, walifaulu mtihani. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika skripti umebainisha kuwa watahiniwa walifaulu vizuri katika mtihani huu kwa kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada zote zilizotahiniwa ikiwa ni pamoja na kutumia lugha kwa usahihi, kuzingatia matakwa ya swali na kutoa hoja sahihi zenye mifano thabiti. Vilevile, sababu mbalimbali za watahiniwa kupata ufaulu wa wastani zimeoneshwa, ikiwa ni pamoja na kutoa majibu yasiyojisheleza au kutoa hoja chache katika majibu yao.

Aidha, pamoja na ufaulu wa jumla wa watahiniwa kuwa juu, sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kupata alama hafifu katika maswali ya mtihani huu zimefafanuliwa. Sababu hizo ni pamoja na kukosa mtiririko mzuri katika majibu yao, kutoandika utangulizi na hitimisho katika maswali ya insha, kukosa weledi wa dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Kiswahili, kuchanganya majina ya mashairi, kushindwa kubainisha vipengele vya kifani katika usanifu wa maandishi, kushindwa kufanya tafsiri kutoka lugha moja kwenda nyingine na kujibu maswali kinyume na matakwa ya maswali.

Mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kupata mbinu za kuboresha ufaulu ili uendelee kuwa wa juu katika mitihani ijayo kwa watahiniwa wote. Baraza la Mitihani la Tanzania linawashukuru wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.

Athumani S. Amasi
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kidato cha Sita uliofanyika mwezi Mei 2022 uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Kiswahili wa Kidato cha Tano na Sita. Mtihani wa somo la Kiswahili ulikuwa na karatasi mbili ambazo ni 121/1 - Kiswahili 1 iliyotahini mada za *Ufahamu na Ufupisho*, *Utumizi wa Lugha*, *Matumizi ya Sarufi*, *Utungaji*, *Maendeleo ya Kiswahili* na *Tafsiri na Ukalimani*; na 121/2 - Kiswahili 2 ambayo ilitahini mada za *Fasihi kwa Ujumla*, *Maendeleo ya Fasihi Simulizi*, *Usanifu wa Maandishi* na *Uhakiki wa kazi za Fasihi Andishi*.

Mtihani wa 121 Kiswahili 1 ulikuwa na sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali manne (4) na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote na, sehemu B ilikuwa na maswali manne (4) na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu, na swali la tano (5) lilikuwa la lazima.

Mtihani wa 121/2 Kiswahili 2 ulikuwa na sehemu A na B. Katika sehemu A mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote na sehemu B ilikuwa na maswali manne (4) na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu (3) ambapo, swali la tano (5) lilikuwa la lazima.

Mtihani wa Kiswahili ulifanywa na watahiniwa wapatao 25,050 ambapo wavulana walikuwa 13,194 na wasichana walikuwa 11,856. Kwa ujumla watahiniwa wote waliofanya mtihani mwaka 2022 walifaulu kwa kiwango cha asilimia 100 kwa kupata daraja A hadi S, ambapo hakuna mtahiniwa aliyepata alama chini ya 35 (daraja F). Jedwali Na. 1 linaonesha ulinganifu wa ufaulu wa watahiniwa kwa kila daraja kwa mwaka 2021 na 2022.

**Jedwali Na. 1: Ufaulu wa Watahiniwa kwa kila Daraja**

| **Mwaka** | **Waliofanya** | Ufaulu (%) | **Gredi za Ufaulu** (%) | | | | | | **Waliofeli** (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **A** | **B** | **C** | **D** | **E** | **S** | **F** |
| 2021 | 20,756 | 100 | 0.78 | 33.24 | 55.42 | 10.02 | 0.53 | 0.02 | 0 |
| 2022 | 24,944 | 100 | 1.59 | 44.42 | 49.38 | 4.47 | 0.13 | 0.01 | 0 |

Katika **Jedwali Na. 1**, takwimu zinaonesha kuwa asilimia ya ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2022 iliongezeka katika daraja A na B, na ilipungua katika daraja C, D, E na S. Hivyo, ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri zaidi kwa mwaka 2022 kuliko mwaka 2021 kwani ufaulu katika madaraja ya juu ulikuwa na watahiniwa wengi zaidi ya yale ya chini. Pia, takwimu katika

miaka hiyo miwili zinaonesha kuwa watahiniwa wengi walifaulu kwa daraja C na hakuna aliyefeli kwa kupata daraja F.

Uchambuzi umefanyika ili kubainisha jinsi maswali yalivyojibiwa, namna yalivyopaswa kujibiwa na changamoto zilizojitokeza. Wakati wa uchambuzi matokeo ya watahiniwa yaliwekwa katika viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni *vizuri*, *wastani* na *hafifu* vilizingatiwa. Kiwango kizuri cha ufaulu ni alama 60 hadi 100, kiwango cha wastani alama 35 hadi 59 na ufaulu hafifu alama 0 hadi 34. Aidha, chati na majedwali mbalimbali yametumika kufafanua viwango vya ufaulu ambapo katika kila chati, rangi nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu, njano inawakilisha ufaulu wa wastani na kijani inawakilisha ufaulu mzuri. Vilevile, sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa katika kila swali ili kuthibitisha maelezo ya uchambuzi.

# 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

Uchambuzi wa majibu kwa kila swali umefanyika ili kuonesha ufafanuzi wa kina wa majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kila swali na kuonesha maswali yaliyofanyika kwa kiwango kizuri, cha wastani na yale yaliyofanyika kwa kiwango hafifu. Aidha, sababu za ufaulu wa watahiniwa zimeelezwa bayana kwa kila swali.

## 2.1 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA

Karatasi ya kwanza imegawanyika katika sehemu A na B. Uchambuzi ulikuwa kama ilivyooneshwa katika sehemu zifuatazo:

### 2.1.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI


Sehemu hii ilikuwa na maswali manne ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama kumi (10).

#### 2.1.1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali lilitoka katika mada ndogo ya Ufahamu *wa Kusoma na Ufupisho* na lilikuwa mahususi katika kupima uelewa wa mtahiniwa katika kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali yaliyohusiana na habari hiyo. Swali lilikuwa na vipengele vinne, (a) - (d) vyenye jumla ya alama 10.

Swali lilimtaka mtahiniwa (a) kuandika kichwa cha habari chenye maneno yasiyozidi matatu; (b) kuorodhesha mawazo makuu matatu yanayopatikana katika aya ya pili, (c) kutaja faida moja ya serikali kusimamia utawala bora na (d) kueleza maana ya maneno (i) Kihoro, (ii) Demokrasia, (iii) Kutaharuki na (iv) Kinyongo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari.

Swali lilijibiwa na watahiniwa 25,050 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri sana ambapo watahiniwa wengi (23,719) sawa na asilimia 94.69 walifaulu kwa kiwango kizuri na wengine kiwango cha wastani. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Katika Chati Na. 1, watahiniwa 1,331 (5.31%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3, watahiniwa 4,600 (18.36%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3.5 hadi 5.5 na watahiniwa 19,119 (76.32%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 6.0 hadi 10.

Ufaulu mzuri wa watahiniwa (76.32%) ulitokana na uelewa wa kifungu cha habari na kuweza kutoa majibu sahihi katika vipengele vingi vya swali hili. Watahiniwa hao waliweza kupendekeza kichwa cha habari kama UHURU, DEMOKRASIA au UHURU NA DEMOKRASIA kwa usahihi. Pia waliorodhesha mawazo makuu matatu yanayopatikana katika aya ya pili kama vile *haki ya mtu ya kuishi bila kubughudhiwa au kunyanyaswa, kutoa maoni/maamuzi yake na kuwasiliana ili mradi asiwe na maneno ya uchochezi*.

Vilevile, watahiniwa hao waliweza kubaini kwa usahihi faida moja ya serikali kusimamia utawala bora ambayo ni *kuwajengea wananchi utayari wa kulihudumia taifa lao kwa dhati na kwa moyo*. Hali kadhalika, walieleza maana sahihi ya kila neno walilopewa kama vile: *kihoro;* huzuni kubwa apatayo mtu kutokana na kupotelewa kitu au jambo fulani, *demokrasia*; mfumo wa uendeshaji wa serikali unaojikita katika kuhimiza na kuruhusu haki stahiki za raia katika kusema, kuabudu na kutoa maoni mbalimbali, *kutaharuki*: hali ya kutokuwa na utulivu na umakini/wasiwasi, mbabaiko au hali ya kusubiri jambo jema/baya linaloweza kutokea na *kinyongo*; hasira za ndani ndani, chuki au mfundo. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyetoa majibu sahihi kwa vipengele (a) hadi (d).



1. a) UMUHIMU WA UHURU

b) Manufaa ya mwananchi

• Mtu binafsi anayo haki ya kuishi bila kubughudhiwa au kunyanyaswa na mtu.

• Mtu anahuru wa kwenda apendapo ili mradi asivunje sheria.

• Mwananchi anao uhuru wa kufanya mawasiliano ya halali ili mradi hatoi matusi ya kum tukana mtu au serikali.


1. c) Faida ya Stiriki kusimamia utawala bora wananchi huwa tayari kutumikia Taifa lao kwa ~~ny~~ moyo mmoja bila kinyongo.

d) Kueleza maana ya maneno yafuatayo.

(i) Kihoro - huzuni

(ii) Demokrasia - haki ya kuishi bila kubughudhiwa na mtu.

(iii) Kutaharuki - ~~Fazba~~ kuhamaki

(iv) Kinyongo - Chuki


Kielelezo Na.1.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 1.1, mtahiniwa alionesha kuwa alielewa kifungu cha habari na kujibu vipengele vyote vinne kwa usahihi. Hata hivyo, katika kuelezea maana za maneno, alitumia misamiati inayohitaji ufafanuzi. Kwa mfano, neno “kutaharuki” aliandika *kutahamaki* badala ya hali ya kutokuwa na utulivu na umakini/wasiwasi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 4,600 sawa na asilimia 18.36 walipata ufaulu wa wastani kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 5.5. Ufaulu huu ulitokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele vya swali. Baadhi ya watahiniwa walitoa maana zisizo sahihi za maneno katika kipengele (d) (i) hadi (iv), wengine waliorodhesha mawazo yasiyo sahihi kulingana na aya ya pili ya habari waliyopewa ili kujibu kipengele (b). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea *athari za ufisadi* kuwa ni jambo ambalo halikugusiwa na mwandishi. Aidha, wapo watahiniwa waliopendekeza kichwa sahihi cha habari katika kipengele (a) lakini kikawa na maneno zaidi ya

matatu kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika "UHURU NA DEMOKRASIA HUMWONDOLEA RAIA TAHARUKI NA KINYONGO," hivyo kupata alama za wastani.

Watahiniwa wachache (5.31%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3 kwa kuwa walishindwa kutoa majibu sahihi katika vipengele vingi. Baadhi ya watahiniwa walionesha kukosa uelewa wa kifungu cha habari, hivyo kupendekeza kichwa cha habari kisichokuwa sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *UKOLONI MAMBOLEO* na mwingine alinakili baadhi ya sentensi zilizopo katika kifungu cha habari katika kujibu kipengele (a); badala ya kuandika kichwa sahihi "UHURU, DEMOKRASIA au UHURU NA DEMOKRASIA." Wapo watahiniwa waliorodhesha mawazo ya mwandishi yasiyo sahihi katika aya ya pili kwa kuandika suala la (i) *uongozi mzuri, (ii) uhuru wa kujitawala* na *(iii) haki za binadamu kwa kuwa na uzalendo katika nchi* ili kujibu kipengele (b) wengine walitaja faida zisizo sahihi kuhusu serikali kusimamia utawala bora kama vile *kusaidia katika kuleta maendeleo katika nyanja ya kiuchumi, kisiasa na kijamii katika nchi*; katika kipengele (c) kinyume na uhalisia uliopo katika kifungu cha habari walichopewa. Aidha, watahiniwa wengine katika kundi hili walikosa ufahamu na uelewa wa misamiati na kutoa maana dhaifu katika kipengele (d) (i) hadi (iv). Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyojitosheleza katika vipengele vingi vya swali hili.



1. (a) UHURU KATIKA MAISHA

b) i) Kuwa mzalendo au wazalendo
ii) Kuepuka kuvunja sheria
iii) Kushiriki katika ujenzi wa jamii

c) i) husaidia kumalisha ulinzi na usalama katika jamii ambapo hupelekea maendeleo ya jamii katika sekta mbali mbali mfano kilimo

d) i) Kihero - Kufa kwa tamaa ambapo tunaona kasuku akipewa uhuru anautumia kupita kiasi

ii) Demokrasio - hali ya kuwa na uhuru mfano kuenda mahali popote pasipo kuvunja sheria za nchi, uhuru wa kutoa maamuzi

iii) Kutaharuki - kuchukia au kukasirika hii ni sifa ya mzalendo

iv) Kinyongo - paspo wasiwasi mfano kushiriki katika shughuli za ujenzi wa taifa


Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1.

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha kuwa, mtahiniwa hakuelewa kifungu cha habari ipasavyo, maana alitoa majibu yasiyo sahihi kwa baadhi ya vipengele hivyo akapata alama za chini.

#### 2.1.1.2 Swali la 2: Utumizi wa Lugha

Swali hili lilitoka katika mada ya *Utumizi wa Lugha* katika mada ndogo ya *Umahiri wa Lugha*. Swali lililenga kupima kumbukumbu na lilimtaka mtahiniwa kueleza mambo muhimu matano yanayoweza kumsaidia mtumiaji wa lugha kuwa mahiri.

Swali lilijibiwa na watahiniwa 25,050, sawa na asilimia 100. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi. Asilimia 97.96 sawa na watahiniwa 24,050 walijibu vizuri swali hili na kufaulu kwa kiwango cha wastani na wengine kwa kiwango kizuri zaidi kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10 mtawalia. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*

Katika Chati Na. 2, watahiniwa 1000 (3.99%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3, watahiniwa 1,512 (6.04%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3.5 hadi 5.5 na wengine 22,538 (89.97%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 6.0 hadi 10.

Watahiniwa wengi (89.97%) walifaulu vizuri kwa kuwa walijibu kwa usahihi swali hili na kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10. Kati yao, 54.3% walijibu vizuri zaidi na kupata alama za juu kuanzia 8.5 hadi 10. Ufaulu mzuri wa watahiniwa hao ulitokana na kuwa na maarifa

kuhusu umahiri katika lugha. Watahiniwa hao waliweza kueleza kwa usahihi mambo muhimu matano yanayoweza kumsaidia mtumiaji wa lugha kuwa mahiri kama vile;

*Matumizi ya mara kwa mara ya lugha ambayo mtu anaifahamu, kusoma maandishi mbalimbali kwa mfano, vitabu vya taaluma, fasihi, majarida na magazeti, kuisomea lugha kwa kiwango cha juu ili kumudu stadi muhimu, kuwakosoa au kuwasahihisha waharibifu wa lugha, kuelewa mila na utamaduni wa jamii husika na kuepuka athari ya lugha nyingine katika lugha anayoitumia mmahiri.*


Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za juu kutokana na kukidhi matakwa ya swali hili.

2 i) Kusomea lugha hiyo kwa kiwango cha juu.
Mtumiaji wa lugha ili aweze kuwa mahiri lazima asome lugha hiyo kwa kiwango cha juu sana ili kuweza kumuwezesha mtumiaji huyo kuwa mahiri wa lugha. Mfano mtumiaji wa lugha ya kiingereza na kiswahili lazima asomee.

ii) Kuwa karibu na watumiaji wa lugha hiyo
Pia ili uweze kuwa mahiri wa lugha lazima uwe na ukaribu sana na watumiaji wa lugha hiyo. Mfano: lugha ya Kiswahili lazima na ukaribu na watumiaji wa lugha hiyo ya Kiswahili.

iii) Kuepuka athari ya lugha nyingine.
Pia mtu ili ~~awe~~ awe mahiri anatakiwa kuepuka athari za lugha nyingine, kama vile lugha mama, hivyo itaweza kumsaidia mtu huyo kuwa mahiri wa lugha hiyo.

iv) Kuwakosoa na kuwasahihisha waharibifu wa lugha.
Pia ili uwe mahiri wa lugha lazima uweze kubaini makosa ya kisarufi, kimuundo na kimtindo au matamshi katika lugha hiyo na kuweza kuwakosoa na kuwasahihisha waharibifu wa lugha hiyo kutokana na hivyo kumfanya mtumiaji wa lugha hiyo husika kuwa mahiri wa lugha.


Q v) Kutumia lugha hiyo kwa matumizi ya kila siku.
Pia katika mambo ya kuzingatia yanayomfanya mtumiaji wa lugha kuwa mahiri ni kuweza kutumia lugha hiyo kwa matumizi ya kila siku. Hivyo kumuwezesha mtumiaji huyo kujua vizuri lugha na kutumia lugha na kuwa mahiri.

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2.


Katika Kielelezo Na. 2.1, mtahiniwa alielezea kinaganaga mambo muhimu matano yanayoweza kumsaidia mtumiaji wa lugha kuwa mahiri.

Aidha, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa kwa swali hili unaonesha kuwa watahiniwa wengine (1,512) (6.04%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kuwa walikuwa na uelewa usiojitosheleza kuhusu mada ya umahiri wa lugha. Watahiniwa hao waliweza kueleza kwa usahihi baadhi ya mambo yanayoweza kumsaidia mtumiaji wa lugha kuwa mahiri. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kwa usahihi mambo muhimu mawili kama vile; *Kusoma lugha hiyo kwa kiwango cha juu* na *kuwa karibu na wazungumzaji wa lugha hiyo.* Aidha, mtahiniwa huyo alitoa hoja nyingine zisizo sahihi kama vile *kutumia lugha ya kiingereza, kukwepa lugha za makabila* na *kutumia nyimbo mbalimbali*; ambapo hazikukidhi matakwa ya swali, hivyo kupata alama za wastani. Mambo muhimu yanayomsaidia mtumiaji wa lugha kuwa mahiri yaliyoachwa na mtahiniwa huyo ni pamoja na *uzalendo katika lugha, kujua sheria na kanuni za lugha husika* na *kuachana na ukasumba.* Kwa ujumla watahiniwa hao walikuwa na majibu yasiyojitosheleza kwa hoja au kwa ufafanuzi.

Licha ya ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swali hili, watahiniwa wachache (3.99%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3. Ufaulu wa chini wa watahiniwa hao ulitokana na kuwa na uelewa mdogo juu ya mada ya umahiri wa lugha, kwani baadhi yao walieleza mambo yanayozingatiwa katika mazungumzo kama vile *mazingira, mada ya mazungumzo, umri wa mzungumzaji, jinsia, Uhusiano wa wazungumzaji* na *vyeo/elimu ya wazungumzaji* badala ya kuelezea mambo muhimu yanayoweza kumsaidia mtumiaji wa lugha kuwa

mahiri. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kujibu swali hili alitoa hoja mseto zinazohusu *dhima za lugha, sifa za lugha na utata katika tungo*, hoja ambazo hazina uhusiano wowote na kiini cha swali hili. Watahiniwa wengine walifafanua makosa mbalimbali yanayoweza kusababishwa na watumiaji wa lugha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika, *kutumia maneno yenye maana zaidi ya moja, kutozingatia matamshi* na *kutozingatia mantiki* badala ya kueleza mambo muhimu yanayoweza kumsaidia mtumiaji wa lugha kuwa mahiri kama vile; *kusomea lugha hiyo kwa kiwango cha juu, kuepuka athari za lugha mama, kuwa karibu na wajuzi wa lugha, kutumia lugha katika matumizi ya kila siku* na *kukosoa/kusahihisha makosa katika lugha husika.* Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

Q2. Umahiri Ni hali au uwezo wa Kutumia
lugha Kwa Kuzingatia stadi zote yaani!
Kuzungumza, Kusoma, Kuandika na Kusikiliza
Yafuatayo ni mambo muhimu matano yana
yoweza Kumsaidia mtumiaji wa lugha Kuwa
mahiri:-
Kutambua ni sauti zipi atakazotumia
Kuunda maneno ya lugha yake; Ni mojawapo ya
jambo ambalo litamsaidia mtumiaji wa
lugha Kuwa mahiri Kutokana na Kutambua
ni sauti zipi atakazotumia Kuunda maneno
itapanga lugha yake Kuwa bora.
Kutambua mpangilio wa vipashio ataka
vyotumia katika lugha yake; Ni mojawapo ya
sababu pia ni lazima ajue mpangilio wa vipa
shio yaani Kikubwa hadi Kidogo ili Kuleta
uwiano Kwenye lugha yake.
Kutambua tungo za Kisarufi za
upatanisho wa Kisarufi: pia ni mojawapo
ya jambo ambalo litampanga mzungumzaji
Kuwa mahiri wa lugha lazima atambue tungo
za Kisarufi ili Kuleta uwiano wa lugha.
Kutambua sentensi tata na namna
ya Kuondoa utata huo; pia ni mojawapo
ya jambo la Kuzingatia ni muhimu Kwa
mzungumzaji Kutambua utata unaojitokeza Kwenye
sentensi husika na Kuondoa utata huo hii itampa
Kuonekana mahiri wa lugha
Kutambua Kwa urahisi Kundi
la sentensi; pia ni mojawapo ya jambo
ambalo mzungumzaji akilitumia atame
Kana Kuwa mahiri wa lugha ni lazima


Q2. awe na uwezo binafsi na waharaka
Kutambua Kusudio la senteni huvika
ili Kumsaidia mzungumzaji Kuwasilisha
dhana inayoeleweka.
Umahiri wa lugha ni muhimu
Sana Katika jamii Kwani husaidia
Kwa Kiasi Kikubwa Kuhakikisha matu
mizi sahihi ya lugha na hata hivyo
husaidia Kutidhi haja ya mawasiliano
Kwa jamii huvika.


**Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 2.2, mtahiniwa alielezea mambo yanayohusiana na matawi ya sarufi kama vile sauti, miundo, mpangilio na maana za maneno katika lugha kwa kuandika *kutambua sauti*, *mfuatano wa vipashio*, *upatanisho wa kisarufi* na *namna ya kutumia na kuondoa utata katika lugha*, kinyume na matakwa ya swali.

### 2.1.1.3 Swali la 3: Utumizi wa Lugha

Swali hili lilitoka katika mada ya *Utumizi wa Lugha* na lililenga kupima kumbukumbu ya mtahiniwa kuhusu matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali. Swali lilikuwa na vipengele vinne vilivyomtaka mtahiniwa kufafanua kwa mifano dhana zifuatazo; (i) Utata katika lugha, (ii) Rejesta, (iii) Misimu (simo) na (iv) Umahiri wa lugha.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 25,050. Uchambuzi unaonesha kuwa swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi ambapo watahiniwa 25,025 sawa na asilimia 99.90 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kiwango cha juu zaidi kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3*

Katika Chati Na. 3, watahiniwa 25 (0.10%) walipata alama hafifu 0 hadi 3, watahiniwa 417 (1.66%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3.5 hadi 5.5 na watahiniwa 24,608 (98.24%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 6.0 hadi 10.

Watahiniwa wengi (98.24%) waliweza kujibu kwa usahihi swali hili na kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Zaidi ya nusu ya watahiniwa wote, 14,119 sawa na asilimia 56.4 walipata alama za juu kuanzia 8.5 hadi 10. Ufaulu mzuri wa watahiniwa hao ulitokana na uelewa wa dhana mbalimbali zinazohusu matumizi ya lugha kwa ujumla hivyo kufafanua kwa usahihi dhana katika kipengele (i) hadi (iv) walizopewa kwa kuandika (i) Utata katika lugha *ni hali ya neno au sentensi kuwa na maana zaidi ya moja na yenye kuleta mkanganyiko katika utumizi wake,* (ii) Rejesta *ni mtindo wa lugha unaotumika katika mazingira maalumu,* (iii) Misimu (simo) *ni maneno yanayozushwa na kikundi cha watu wenye utamaduni mmoja ambayo huzuka na kutoweka na mengine husanifiwa na kuwa lugha rasmi* na (iv) Umahiri wa lugha *ni ujuzi wa hali ya juu katika stadi kuu nne ambazo ni kusoma, kuandika, kusikiliza na kuzungumza.* Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

03 Zifuatazo ni ufafanuzi wa dhana zifuatazo

i- Utata katika lugha ni hali ya neno au sentensi kuwa na maana zaidi ya moja

Mfano ni mbuzi, Paa, kima, mfano katika sentensi ni Juma anaendesha, Amina amenipi gia mpira


ii- Rejesta ni mtindo wa lugha unaotumika penyo shughuli fulani ambao ni tofauti na lugha ya kawaida kuna aina za rejesta kama vile rejesta za mitaani, rejesta za mahali, rejesta zinazohusu watu Mfano wa rejesta za mahali Mchungaji: bwana yesu asifiwe

Waumini : Amen

Mchungaji: Tumsifu yesu kristo

Waumini : milele amina

iii- Simo (misimu) ni maneno yasiyo sanifu yanayozushwa na kikundi fulani cha watu wenye utamaduni mmoja katika jamii, kuna aina za misimu ni misimu za gao, misimu za pekee na misimu za gao ambazo hizi huvuka mipaka ya nchi. Mfano wa misimu Mimi nafunga ofisi


03 Mshikaji naamcha ndege, Mshikaji ninaaway
a tu


iv- Umahiri wa lugha ni uzuri wa utumiaji wa lugha katika stadi nne za lugha kama kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika. mfano umahiri wa lugha katika kingereza, I enjoy to play football, She likes to eat banana. umahiri katika lugha ya kindali mfano Utata ikulima, Umundu alikulya bhugali

Kielelezo Na. 3.1**:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3.

Katika Kielelezo Na. 3.1, mtahiniwa alifafanua (i) *Utata katika lugha,* (ii) *Rejesta,* (iii) *Simo (misimu)* na (iv*) Umahiri wa Lugha* kwa usahihi na kutumia mifano sahihi kulingana na matakwa ya swali.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 417, sawa na asilimia 1.66, walipata alama kuanzia 3.5 hadi 5.5. Ufaulu wa wastani wa watahiniwa hao ulitokana na ufafanuzi usiojitosheleza kwa baadhi ya dhana za matumizi ya lugha walizopewa. Baadhi ya watahiniwa waliweza kufafanua dhana walizopewa lakini hawakuweza kutumia mifano sahihi katika baadhi ya vipengele hivyo kupata alama za wastani. Wengine walitoa ufafanuzi usiokidhi matakwa ya swali kwa kutoa maelezo yasiyofafanua vizuri dhana mbalimbali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua rejesta kuwa ni *huduma zinazotolewa posta ili kusafirisha barua/mzigo kutoka sehemu moja hadi nyingine* badala ya *mtindo* wa lugha unaotumika katika mazingira maalum. Mtahiniwa mwingine alifafanua *simo* (*misimu*) kama tanzu mbalimbali za semi katika fasihi simulizi kama vile *methali, vitendawili na misemo* badala ya kueleza kuwa ni maneno yanayozushwa na kikundi cha watu wenye utamaduni mmoja ambayo huzuka na kutoweka na mengine husanifiwa na kuwa lugha rasmi. Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa hao walikosa umahiri wa dhana hizo, hivyo kupata alama za wastani.

Asilimia ndogo sana, (0.10%) ya watahiniwa walipata alama hafifu kuanzia 0 mpaka 3 kutokana na kushindwa kufafanua dhana za utumizi wa lugha walizopewa. Baadhi yao walitoa ufafanuzi wa dhana usiojitosheleza kwa vipengele vingi na wengine walitoa mifano pekee bila kutoa ufafanuzi wowote, hivyo kupata alama za chini. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea umahiri wa lugha kuwa ni *uwezo wa kuzungumza kiingereza* ambapo alitoa mfano wa watoto wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kuwa ndio mahiri *badala ya* kuelezea kuwa ni ujuzi wa hali ya juu wa mtu katika stadi kuu nne ambazo ni kusoma, kuandika, kusikiliza na kuzungumza lugha yoyote. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama hafifu.


3 Jinsia; yampasa mtu kuzingatia
jinsia wakati wa mazungumzo kwa
mba kama ni jinsia ya kiume ajue
atumie lugha gani ili aweze kuwa
mahiri wa lugha pia kama jinsia
ni ya kike ajue azungumze vipi
Uhusiano na unayezungumza
naye; mtu pia inampasa kuzingatia
a uhusiano alionao na mtu anaye
zungumza naye kama ni mzazi basi
atumie lugha ipi katika mawasili
ano hayo.
Cheo cha elimu na unaye
zungumza naye; mmahiri wa lugha
yoyote ile inampasa ajue na kutewa
kuamba je anaezungumza naye je
anacheo gani cha elimu ni msomi
au siyo msomi na baada ya kuju
a hayo ndipo aweze kuchagua lug
ha ya kuzungumza nae
Hivyo, Umahiri wa lugha
pia unaathiri lugha kama katika
nyia tofauti kama vile kimatamshi
lugha inaathiriwa, kimaana, kimtin
do na hata kimuundo pia lugha
kuweza kuathiriwa.

Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3.

Katika kielelezo Na. 3.2, mtahiniwa alifafanua *mambo muhimu ya kuzingatiwa katika mazungumzo* kinyume na matakwa ya swali badala ya kufafanua dhana za utumizi wa lugha alizopewa jambo linalodhihirisha kuwa hakuelewa matakwa ya swali.

#### 2.1.1.4 Swali la 4: Matumizi ya Sarufi

Swali hili lilitoka katika Mada ya *Matumizi ya Sarufi*, mada ndogo ya *Matumizi ya Mofimu.* Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutumia mofimu mbalimbali katika maneno. Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha dhima za mofimu zilizopigiwa mstari katika maneno: (i) *<u>M</u>kimbizi (ii) <u>Hu</u>nun'gunika (iii) Asi<u>ye</u>ridhika (iv) Watembea<u>o</u> (v) Ame<u>ni</u>alika (vi) <u>N</u>imekufikia (vii) Tume<u>ji</u>takia (viii) Wata<u>m</u>furahisha (ix) Pang<u>u</u>a*.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (25,050) waliofanya mtihani huu. Kati yao, watahiniwa 15,387 sawa na asilimia 61.43, walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kiwango cha juu zaidi kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa**


| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0.0 - 3.0 | 9,663 | 38.57 |
| 3.5 - 5.5 | 10,957 | 43.74 |
| 6.0 - 10.0 | 4,430 | 17.68 |


Katika Jedwali Na. 2, watahiniwa 9,663 (38.57%) walipata alama hafifu 0 hadi 3, watahiniwa 10,957 (43.74%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3.5 hadi 5.5 na watahiniwa 4,430 (17.68%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6 hadi 10.

Watahiniwa wengi (43.74%) walifaulu kwa kiwango cha wastani na kupata alama kuanzia 3.5 hadi 5.5. Watahiniwa hao walitoa majibu yasiyojitosheleza katika kubainisha dhima za mofimu zilizopigiwa mstari katika maneno waliyopewa. Hii ilitokana na kukosa umahiri wa

kutosha katika dhana nzima ya uambishaji, hivyo kushindwa kubaini kwa usahihi dhima za mofimu kwa baadhi ya vipengele. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kipengele (i) *m̲kimbizi* alieleza mofimu hiyo kama *nomino* kinyume na matakwa ya swali ambapo–*m-* ni kiambishi kinachoonesha umoja na ngeli. Hali kadhalika, mtahiniwa mwingine katika kipengele (v) *amen̲i̲alika* alielezea mofimu hiyo kama *kitenzi* badala ya kuwa –ni- ni kiambishi rejeshi cha mtenda, hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa 4,430 (17.68%) walifaulu vizuri na kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa dhana ya uambishaji, hivyo kubainisha kwa usahihi dhima za mofimu zilizopigiwa mistari katika maneno waliyopewa katika vipengele vingi. Watahiniwa walibainisha dhima hizo kama ifuatavyo: (i) *m* – kuonesha umoja na ngeli, (ii) *hu-* hali ya mazoea, (iii) *ye* - kirejeshi cha mtenda, *(iv) o* - kirejeshi cha mtendwa (v) *ni* - *kirejeshi cha mtenda*, (vi) *ni* - nafsi ya kwanza umoja/uyakinishi, (vii*)-ji-*kirejeshi cha watenda (viii) *m* - kirejeshi cha mtendwa na (ix) *u* - tendua/kinyume. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha kwa usahihi mofimu saba (7) katika maneno aliyopewa na kupata alama za juu kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 4.1.


04. i. Mkimbizi.
Dhima: Kuonesha umoja.
ii. Hunung'unika.
Dhima: Kuonesha hali ya mazoea.
iii. Asiyendhika.
Dhima: Kuonesha urejeshi wa mtenda.
iv. Watembea.
Dhima: Kuonesha urejeshi wa watenda.
v. Amenialika.
Dhima: Inarejelea mtendwa wa jambo.


04. vi. Nimekupikia.
Dhima: Kuonesha nafsi ya kwanza umoja.

vii. Tumejitakia.
Dhima: Kuonesha hali ya kujirejelea au urejeshi wa watenda.

viii. Watamfurahisha.
Dhima: Kuonesha urejeshi wa mtendewa.


ix. Pangua.
Dhima: Kuonesha kauli ya kutenduka.

Kielelezo Na. 4.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.1, mtahiniwa alibainisha kwa usahihi dhima ya mofimu katika vipengele (i), (ii), (iii), (vi) na (vii) na (ix) lakini alishindwa kufanya hivyo katika vipengele (iv), (v) na (viii).

Kwa upande mwingine watahiniwa 9,663 sawa na asilimia 38.57 walishindwa kubainisha dhima za mofimu zilizopigiwa mistari katika maneno waliyopewa. Kati yao, watahiniwa 1,200, sawa na asilimia 4.8, walipata alama 0 kutokana na sababu mbalimbali. Baadhi hawakuelewa matakwa ya swali hili, hivyo kubainisha neno zima badala ya mofimu stahiki. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alionesha kategoria ya neno kwa kuandika katika kipengele (i) *nomino* na (ii - ix) *kitenzi* badala ya kubainisha dhima ya mofimu walizopewa. Watahiniwa wengine walionesha kukosa uelewa wa dhana ya uambishaji hivyo kushindwa kubainisha kwa usahihi dhima za mofimu walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu yafuatayo: (i) –**m**- *nafsi ya kwanza – umoja,* (ii) -**hu**- *ukanushi,* (iii) -**ye**- *o rejeshi elekezi,* (iv) -**o**- *Kiambishi tamati maana,* (v) -**ni**- *kiunganishi,* (vi) -**ni** – *upatanisho wa kisarufi,* (vii) -**ji** – *kiambishi awali kijenzi,* (viii) -***m*** *– nafsi ya pili wingi* na (ix) **u**- *kiambishi tamati maana*. Majibu haya hayakuwa sahihi, jambo linaloonesha dhahiri kuwa mtahiniwa huyo hakuelewa matakwa ya swali na pia hakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana nzima ya dhima za mofimu.

Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.



04 (i) Imeonesha nomino au jina
(ii) Imeonesha kitendo au tabia ya kitu
(iii) Imeonesha ukanushi
(iv) mofimu O imeonesha au imesimama kuimarisha kielezi
(v) Imeonesha kitenzi au kutenduliwa
(vi) Inaelezea wakati uliopo timilifu
(vii) Inaonesha hali ya kujitendea
(viii) Mofimu M inaonesha hali ya kutendea
(ix) Inaonesha hali ya ukanushi

Kielelezo Na. 4.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.2, mtahiniwa alibainisha dhima zisizo sahihi za mofimu katika vipengele (i) – (ix) na kupata alama hafifu.

### 2.1.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAREFU


Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali manne ya insha. Swali la nane (8) lilikuwa ni la lazima. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu na kila swali lilikuwa na alama 20.

#### 2.1.2.1 Swali la 5: Uandishi wa Barua Rasmi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Utungaji*, mada ndogo ya *Uandishi wa Barua* na lililenga kupima uundaji. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika barua ya kiofisi yenye lengo la kukiri kupokea bidhaa alizoagiza kutoka kampuni ya Mchumi Traders wa S.L.P 750 Mwanza. Bidhaa hizo ni jozi 50 za viatu vya ngozi, jozi 100 za soksi nyeupe, dazeni 100 za penseli, katoni 100 za sabuni ya mbuni na seti 150 za vikombe vya plastiki. Jina lake liwe Malingumu Sulubu wa S.L.P 1000 Magu.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa swali hili lilijibiwa na watahiniwa 21,031 (83.96%) kati ya watahiniwa

wote waliofanya mtihani. Swali hili ndiyo lililojibiwa vizuri zaidi ambapo watahiniwa 21,015 sawa na asilimia 99.92 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama 7 hadi 20. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Katika Chati Na. 4, watahiniwa 16 (0.08%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5, watahiniwa 342 (1.63%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 20,673 (98.30%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa wengi (98.3) walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uandishi wa barua za kiofisi. Watahiniwa 11,653' sawa na asilimia 55.4, walijibu vizuri zaidi swali hili na kupata alama za juu 18 hadi 20. Kwa ujumla, watahiniwa hao waliweza kuandika barua iliyozingatia vyema vigezo vyote muhimu kama vile; anwani ya mwandishi inayokuwa juu upande wa kulia, tarehe chini ya anwani ya mwandishi, anwani ya mwandikiwa inayokuwa juu upande wa kushoto, mwanzo wa barua unaozingatia uhusiano wa kikazi wa mwandishi na mwandikiwa, kichwa cha barua, kiini cha barua, matumizi sahihi ya alama za uandishi, salamu za maagano, saini ya mwandishi na jina la

mwandishi. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali hili.


5
MALINGUMU SULUBU,
S.L.P 1000,
MAGU.
09/05/2022.

KAMPUNI YA
MCHUMI TRADERS
S.L.P 750
MWANZA.

Ndugu,

YAH: KUKIRI KUPOKEA BIDHAA ZILIZOAGIZWA KUTOKA KATIKA KAMPUNI YA MCHUMI TRADERS

Husika na kichwa cha habari tajwa hapo juu. Mimi ni Mfanyabiashara kutoka Magu. Ninakiri kupokea bidhaa zifuatazo
(a) jozi 50 ya viatu vya ngozi
(b) jozi 100 za soksi nyeupe
(c) katoni 100 za penseli
(d) katoni 100 za sabuni ya mbuni, na
(e) seti 150 za vikombe vya plastiki.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa uaminifu wa kampuni yako kwani nimepokea bidhaa hizo zikiwa salama kabisa.


Wako katika ujenzi wa taifa
M. Sulubu
Malingumu Sulubu (mfanyabiashara)

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5.

Katika Kielelezo Na. 5.1, mtahiniwa aliweza kuandika barua ya kukiri kupokea bidhaa zilizoagizwa katika kampuni ya Mchumi Traders kwa usahihi na kupata alama za juu, jambo linaloonesha kuwa alielewa vizuri matakwa ya swali na alikuwa na umahiri katika uandishi wa barua za kikazi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (1.71%) walikuwa na ufaulu wa wastani hadi hafifu. Majibu ya watahiniwa katika kundi hili yanaonesha kutokujitosheleza kwa baadhi ya mambo muhimu ya kuzingatiwa katika uandishi wa barua ya kiofisi. Watahiniwa hao walishindwa kuandika barua ya kukiri kupokea bidhaa zilizoagizwa

kutoka kampuni ya Mchumi Traders wa S.L.P 750 Mwanza. Baadhi yao waliandika barua yenye vipengele sahihi vya barua ya kikazi/ kiofisi kama vile *anwani ya mwandishi*, *tarehe*, *mwanzo wa barua*, *sahihi na jina* na *mwandishi* lakini walishindwa kuandika kwa usahihi baadhi ya vipengele kama vile, anwani ya mwandikiwa inayokuwa upande wa kushoto sambamba na tarehe, kichwa cha barua, kiini cha barua na kutokuwa na salamu za maagano. Hivyo, walikidhi sehemu ndogo tu ya matakwa ya swali na kupata alama za chini. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika barua isiyozingatia muundo wa barua za kikazi/ kiofisi kwa kuandika kichwa cha barua na mwanzo wa barua kwa usahihi na kushindwa vipengele vingine vyote. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa wa aina hiyo.


5 MCHUMI TRADERS SLP 750 MWANZA
YAH: KUKIRI KUPOKEA BARUA KUTOKA KWENYE KAMPUNI YAKO.
Mimi Malingumu Salubu ninakiri kuwamba kampuni
yako iliniturmia bidhaa zifuatazo:
Jozi 50 za viatu vya ngozi, jozi 100 za soksi nyeupe, darzeni
100 za penseli, katoni 100 za sabuni ya mbuni na seti 150
za vikombe vya plastiki, ninakiri bidhaa kuwamba nimeipokea
na ninakiri kuwamba mzigo wote umenifikia ukiwa salama bila
ya upotevuwa kitu chochote kile kati ya niliyoagiza
MALINGUMU SULUBU S.L.P 1000 MAGU.


Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5.

Katika Kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa aliandika barua isiyozingatia vipengele vya barua ya kiofisi kama vile anwani ya mwandishi, tarehe, anwani ya mwandikiwa, mwanzo wa barua na kiini cha barua, matumizi sahihi ya alama za uandishi, salamu za maagano, saini ya mwandishi na jina la mwandishi.

### 2.1.2.2 Swali la 6: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili*, mada ndogo ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili kabla ya Uhuru*. Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kutathmini mchango wa serikali katika kukuza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri sana ambapo watahiniwa 23,022 walilijibu. Kati yao, watahiniwa 22,992 sawa na asilimia 99.87, walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kiwango cha juu zaidi kwa kupata alama kuanzia 7 hadi 20 kama inavyoonekana katika Chati Na. 5.




**Chati Na.** ***5:*** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Katika Chati Na. 5, watahiniwa 30 (0.13%) walipata alama hafifu 0 hadi 6.5, watahiniwa 919 (3.99%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 22,073 (95.88%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.


Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa wengi (95.88%) walijibu vizuri swali hili na kupata alama kuanzia 12 hadi 20. Miongoni mwao, asilimia 9.2 walipata alama za juu zaidi kuanzia 18 hadi 20 kutokana na kufafanua kwa usahihi mchango wa serikali katika kukuza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru. Watahiniwa hao walifafanua namna serikali ilivyochagua Kiswahili kuwa lugha ya taifa, kukitumia katika shughuli za elimu, kisiasa, kidini, kibiashara na kuunda vyombo mbalimbali kwa ajili ya kukuza lugha hii. Kielelezo

Na. 6.1 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

6. Kiswahili ni lugha ya taifa ya Tanzania na ni lugha ya Umoja wa Jumuiya za nchi za Afrika Mashariki. Baada ya kupata Uhuru, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye alikuwa ni waziri mkuu wa kwanza wa Tanganyika na baadae rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipa hadhi lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya Taifa. Hadi sasa lugha ya Taifa ya Tanzania ni Kiswahili. Hata hivyo Kiswahili kinatumika katika Umoja wa nchi za Ukanda wa jangwa la Sahara yaani SADC kama lugha ya mawasiliano baina ya nchi mbambali zinazounda ukanda huo. Ufuatao ni mchango wa serikali katika kukuza Kiswahili Tanzania baada ya Uhuru:-

Kiswahili kuteuliwa kuwa lugha ya taifa, baada ya kupata uhuru mwaka 1961 Serikali ya Tanganyika iliteua lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya taifa. Hata hivyo baada ya kuteuliwa lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya taifa imesaidia sana Kiswahili kuweza kukua na kuenea kwa kasi katika sehemu mbalimbali za nchi yetu. Hivyo basi Serikari imechangia kwa kiasi kubwa sana Kiswahili kuenea katika sehemu mbalimbali za nchi yetu.

Serikali imesaidia au imechangia kukuza Kiswahili kupitia vyombo vya habari, Mfano mzuri katika televisheni ya Taifa TBC redio ya taifa TBC fm, hivyo basi kutoka kuanzishwa taasisi hizi serikali ya Jamhuri ya Muungano imesaidia kukuza na kueneza Kiswahili katika sehemu mbalimbali nchini mijini na vijijini.



6. Serikali imechangia kukuza Kiswahili Katika suala la elimu, Katika suala la elimu Serikali imesaidia sana Kiswahili kuweza kutumika kama lugha ya kufundishia kwa shule za msingi na pia kama somo kwa shule za sekondari, na elimu ya juu. Hivyo basi suala la elimu limesaidia sana kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania baada tu ya kupata uhuru mnamo mwaka 1961.

Lugha ya Kiswahili kutumika katika - shughuli za utawala, vilevile Kiswahili kinatumika katika shughuli za utawala mfano, mzuri ni Bungeni lugha ya Kiswahili inatumika bungeni kama lugha ya mawasiliano. Katika kuwasilisha mambo mbalimbali bungeni yanayotokana na wate wa jimbo husika mfano; kama ukosefu wa maji safi na salama, ukosefu wa umeme. Hivyo basi lugha ya Kiswahili kutumika katika shughuli za utawala imesaidia kukuza Kiswahili na kiweze kuenea katika sehemu mbalimbali za nchi yetu

Serikali imechangia kukuza lugha ya Kiswahili katika siasa, Katika siasa serikali inasisitiza matumizi ya Kiswahili ili kiweze kuendelea kutumika katika sehemu mbalimbali na maeneo mbalimbali katika nchi nzima. Hivyo basi katika suala la siasa lugha inayotumika lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili inatumiwa au inatumika katika siasa ili kuweza kujinadi katika kampeni mbalimbali za uongozi. Kwahiyo ni muhimu sana kuwepo na msisitizo kama huu ili lugha ya Kiswahili izidi kudumu


Kielelezo Na. 6.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 6.

Katika Kielelezo Na. 6.1, mtahiniwa alifafanua kwa usahihi hoja zinazoonesha mchango wa serikali katika kukuza Kiswahili nchini

Tanzania baada ya uhuru na pia aliweza kuthibitisha hoja hizo kwa kutumia mifano na kupata alama za juu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 919 sawa na asilimia 3.99 ya waliojibu swali hili, walipata alama za wastani kuanzia 6.5 hadi 11.5. Majibu ya watahiniwa hao yalikuwa hayajitoshelezi kutokana na kukosa uelewa wa kutosha kuhusu mchango wa serikali katika kukuza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru. Baadhi ya watahiniwa walibainisha hoja sahihi lakini hawakufafanua kama ilivyostahili, hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja hoja zifuatazo; *Kiswahili kutumika katika kampeni za kisiasa, Kiswahili kutumika kama lugha ya taifa, Kiswahili kuteuliwa kama lugha ya kufundishia, kuanzishwa kwa asasi za Kiswahili, Kiswahili kutumika katika vyombo vya habari.* Lakini hakufafanua namna michango hiyo ilivyotumiwa kwa lengo la kukuza Kiswahili, hivyo kupata alama za wastani. Watahiniwa wengine, kutokana na kukosa uelewa wa mada hii ya kukua na kuenea kwa Kiswahili baada ya uhuru, walichanganya hoja zinazothibitisha kukua na kuenea kwa Kiswahili kabla ya uhuru kama vile ujio wa Waarabu, Waingereza na Wajerumani ambao kiuhalisia baadhi ya shughuli zao zilikuza Kiswahili kabla ya uhuru.

Licha ya ufaulu mzuri katika swali hili, watahiniwa wachache (0.13%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kutokana na kukosa umahiri katika mada ya kukua na kuenea kwa Kiswahili. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mchango wa serikali katika kukuza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru. Mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zifuatazo: *kuimarisha utawala, shughuli za kimahakama* na *ujenzi wa miundombinu* ambapo ufafanuzi wake hakuonesha ni kwa namna gani shughuli hizo zimechangia katika kuikuza lugha ya Kiswahili. Hali kadhalika, watahiniwa wengine walichanganya mambo yaliyokuza na kueneza Kiswahili kabla ya uhuru na baada ya uhuru. Mtahiniwa mwingine alielezea ujio wa wageni mbalimbali na shughuli walizofanya kama vile shughuli za kidini, elimu na utawala kama mchango wa serikali katika kukuza Kiswahili kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata alama hafifu.



6. Kiswahili ni lugha inayozungumzwa pwani ya Afrika mashariki. lugha hii ina nadharia mbalimbali zinazoeleza kuhusu chimbuko au asili yake nadharia hizo ni kama vile Kiswahili chimbuko lake ni kiarabu. zifuatazo ni hoja zinazothibitisha kuwa kiswahili ni kiarabu kama ifuatavyo.

Jina lenyewe kiswahili limetokana na kiarabu. kunaona uthibitisho wa kwanza ni jina lenyewe kiswahili ambalo limetokana na neno "sahil" baadaye kutokana na athali za lugha mama kwa kuwa swahili na baada ya lugha kufanyiwa usanifishaji kwa kuwa kiswahili kutokana na jina kiswahili kuloeka katika lugha ya kiarabu basi wanadai kiswahili ni kiarabu.

Msamiati mingi ya kiswahili imetokana na kiarabu. pia kigezo kingine wanachotumia waarabu kuthibitisha kuwa kiswahili kimetoka na na wao ni kuwepo kwa misamiati mingi ya kiarabu katika kiswahili mfano shukrani, salamu, rehema na menginenyo kwa hiyo waarabu wanadai kuwa kiswahili kimetokana na lugha yao kutokana na misamiati mingi ya kiswahili.

Waarabu walirishi pwani ya Afrika mashariki ambako kiswahili kilianzia


Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 6.

Katika Kielelezo Na. 6.2, mtahiniwa alielezea chimbuko la Kiswahili kutokana na ujio wa Waarabu ambao walikuza Kiswahili kwa misamiati yao na shughuli mbalimbali walizozifanya katika upwa wa Afrika Mashariki kinyume na matakwa ya swali.

#### 2.1.2.3 Swali la 7: Asili ya Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili*, mada ndogo ya *Asili ya Kiswahili*. Swali lilimtaka mtahiniwa kutathmini dai kuwa asili ya Kiswahili ni kiarabu kwa kutumia hoja tatu kisha kuonesha udhaifu wa dai hilo kwa kutoa hoja tatu.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 6,044 (24.1) kati ya 25,050 waliofanya mtihani huu. Kati yao, watahiniwa 5,897 sawa na asilimia 97.57, walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kiwango cha juu kwa kupata alama kuanzia 7 hadi 20 kama inavyoonekana katika Chati Na. 6.




**Chati Na.** ***6:*** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Chati Na. 6, inaonesha kuwa watahiniwa 147 (2.43%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5, watahiniwa 682 (11.28%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 7 hadi 11.5 na 5,215 (86.28%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa wengi (86.28%) waliojibu swali hili waliweza kupata alama za juu kuanzia 12 hadi 20 kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili. Miongoni mwao, watahiniwa 976 sawa na asilimia 16.1 walitoa majibu toshelevu na kupata alama 18 hadi 20. Watahiniwa hao waliweza kutoa hoja sahihi zinazothibitisha kuwa asili ya Kiswahili ni kiarabu kama vile; *neno lenyewe "Kiswahili" limetokana na kiarabu, istilahi/misamiati mingi ya lugha ya Kiswahili ni ya kiarabu* na *suala la dini ya kiislamu iliyojikita katika kiarabu kwa kiasi kikubwa.*

Aidha, watahiniwa hao waliweza pia kutoa hoja sahihi zinazoonesha udhaifu wa madai hayo yanaoonesha kuwa asili ya Kiswahili ni kiarabu kama vile; *suala la dini halitoshelezi uwepo wa lugha maalum, asili ya kiarabu katika Kiswahili limeegemea zaidi upande wa msamiati* na *kupuuza suala la miundo ya sentensi* na *kutokuonesha lugha iliyokuwa ikitumiwa na watu wa pwani ya Afrika Mashariki kabla ya ujio wa waarabu.* Aidha, watahiniwa hao walitoa utangulizi na hitimisho linaloendana na swali. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za juu katika swali hili.

7. Asili ya Kiswahili ni namna au jinsi Lugha ya Kiswahili ilivyoanza kutumika. Kuna nadharia za aina mbalimbali zinazoeleza asili ya Lugha ya Kiswahili mfano asili ya Kiswahili ni Kongo na asili ya Kiswahili ni pijini au krioli. Kuna nadharia ya Kiarabu ambayo hudai kuwa asili ya Kiswahili ni Kiarabu hii inajidhihirisha kupitia hoja kuu tatu ambazo ni :-

Neno lenyewe la Kiswahili ni la kiarabu, nadharia ya kiarabu inadai kuwa neno Kiswahili limetokana na kiarabu asili yake mfano neno "sahel" likiwa na maana ya umoja na "swahili" likiwa na maana ya wingi kwa ujumla maneno hayo yenye asili ya kiarabu yanaunda neno Kiswahili hivyo nadharia hii hujikita zaidi kuangalia jina la Lugha yenyewe ya Kiswahili na kudai kuwa asili ya Lugha ya Kiswahili ni Kiarabu.


Misamiati mingi ya Kiswahili ni ya kiarabu Nadharia ya kiarabu hudai kuwa uwepo wa misamiati mbalimbali ya kiarabu kama vile Madrasa, shekhe ni uthibitisho tosha kuwa Lugha ya

7. Kiswahili imetokana na Kiarabu hivyo nadharia hii hujikita zaidi kuangalia uwepo wa Msamiati ya Kiarabu kwenye lugha ya Kiswahili hivyo hudai kuwa Kiswahili kimetokana na Kiarabu kwa kuangalia kigezo cha Msamiati au wingi wa maneno.

Uwepo wa dini ya Kiislamu, nadharia hii inadai kuwa kwa kuwa Kiswahili kilianza pwani ya Afrika Mashariki na idadi kubwa ya wakazi ni waislamu, na kwa kuwa uislamu ulileta na waarabu basi hata Kiswahili nacho kililetwa na waarabu mfano ni Tanzania hivyo nadharia hii inajikita zaidi kwenye dini wakiamini kuwa ujio wa dini ya Kiislamu ulifuatana na Kiswahili. Licha ya madai haya nadharia ya Kiarabu imeonekana kuwa na udhaifu kwenye madai yake udhaifu huo ni:-

Lugha haiwezi kuwa lugha kwa sababu ya dini hii au imani, imani haitoshi kueleza chimbuko na asili ya lugha ya Kiswahili kuwa ni Kiarabu kwani pwani ya Afrika Mashariki ilipata kutumia Kiswahili hata kabla ya ujio wa dini ya Kiislamu hivyo sio kweli kujadili asili ya Kiswahili kuwa ni Kiarabu kwa kutumia dini ya Kiislamu kiuhalisia lugha haitokani na imani ya watu.

Lugha ya Kiswahili ina Msamiati mingi ya lugha mbalimbali kwani ni tabia ya lugha kuwa na maneno ya lugha tofauti tofauti, uthibitisho wa asili ya Kiswahili kwa kutumia kigezo cha Msamiati sio sahihi kwani kila lugha hukopa na kutohoa maneno kutoka lugha mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya wazungumzaji hivyo kupitia Msamiati ya lugha ya Kiarabu kama thamani, thelathini na thumuni haitoshi kueleza kuwa chimbuko na asili ya Kis


7. Kiswahili ni kiarabu hivyo ni tabia kwa kila lugha kuwa na maneno kutoka lugha tofauti tofauti.
Asili ya lugha haiwezi kupimwa kwa jina la lugha husika, lugha ya Kiswahili haiwezi kuwa ni kiarabu kwa sababu ya neno Kiswahili hivyo dai hili linakosa mashiko ya kueleza asili ya lugha ya Kiswahili kuwa ni kiarabu kutokana na kushindwa kushawishi na kutoa uthibitisho wa kisayansi ambao unahusisha elimu au ushahidi wa kihistoria unaoonyesha asili ya lugha hivyo haitoshi kueleza Kiswahili kuwa ni kiarabu kwa kutumia jina.
Kwa ujumla, nadharia ya kiarabu imekuwa na mchango mkubwa juu ya kuendeleza mjadala wa kutafuta asili ya Kiswahili kwani nadharia hii imepelekea kuibuka kwa nadharia ya kibantu ambayo imeweza kutoa ushahidi wa kisayansi na kihistoria juu ya asili ya Kiswahili na kuonekana kuwa na mashiko zaidi kuliko nadharia ya kiarabu iliyoshindwa kutoa ushahidi wa kisayansi au wa kihistoria.

Kielelezo Na. 7.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 7.

Watahiniwa 682 sawa na asilimia 11.28 walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5. Baadhi ya watahiniwa waliweza kutumia hoja tatu sahihi kujadili dai linalohusu asili ya lugha ya Kiswahili kuwa ni kiarabu lakini walishindwa kuonesha udhaifu wa madai hayo kwa kutumia hoja tatu. Vilevile, watahiniwa wengine waliweza kujadili kwa usahihi hoja pungufu zinazoonesha kuwa Kiswahili ni kiarabu kama vile; *neno Kiswahili linatokana na neno la kiarabu Sahel* na *lugha ya Kiswahili kubeba zaidi ya asilimia 30 ya maneno ya kiarabu*. Hata hivyo, walishindwa kujadili hoja zinazohusiana na ujio wa waarabu katika pwani ya Afrika Mashariki ambako Kiswahili kilianzia na hoja nyinginezo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (2.43%) waliojibu swali hili walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama 0 hadi

6.5. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walishindwa kutoa hoja tatu za madai kuwa Kiswahili ni Kiarabu na kuonesha udhaifu wa madai hayo. Baadhi ya watahiniwa walionesha kukosa uelewa kuhusu asili ya Kiswahili hivyo, kushindwa kujadili madai kuwa Kiswahili ni kiarabu badala yake walieleza hoja kama*; biashara, elimu na ndoa* bila kuzihusisha na mchango wa waarabu katika kukuza Kiswahili katika maeneo ya Afrika Mashariki. Watahiniwa wengine walionesha kutokuelewa matakwa ya swali hili, hivyo kushindwa kuonesha udhaifu wa madai ya asili ya Kiswahili kuwa ni Kiarabu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia hoja zifuatazo; *msamiati wa msingi*, *nomino za Kiswahili* na *tungo za Kiswahili* ambazo kiuhalisia ni hoja zinazothibitisha kuwa Kiswahili ni kibantu na sio udhaifu wa madai ya asili ya Kiswahili kuwa ni Kiarabu. Kwa ujumla, watahiniwa hao walitakiwa kujadili madai ya kuwa asili ya Kiswahili ni Kiarabu kama vile *neno lenyewe "Kiswahili" limetokana na kiarabu*, *istilahi/misamiati mingi ya lugha ya Kiswahili ni ya Kiarabu* na *suala la dini ya kiislamu iliyojikita katika Kiarabu kwa kiasi kikubwa.* Aidha, watahiniwa hao walitakiwa pia kuonesha udhaifu wa madai kuhusu asili ya Kiswahili kuwa ni kiarabu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kundi hili alijibu swali hili vibaya kwa kutoa hoja zisizo sahihi katika kuonesha udhaifu kuwa Kiswahili ni Kiarabu kwa kuandika "hakuna udhaifu wowote kwani Kiswahili kinatokana na Kiarabu. Mtahiniwa huyo alitakiwa kuelezea hoja kama vile: *suala la dini ya kiislam halitoshelezi uwepo wa lugha maalum, asili ya Kiarabu katika Kiswahili limeegemea zaidi upande wa msamiati* na *kupuuza suala la miundo ya sentensi* na *dai hilo kutokuonesha lugha iliyokuwa ikitumiwa na watu wa pwani ya Afrika Mashariki kabla ya ujio wa waarabu.* Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuthibitisha dai kuwa Kiswahili ni Kiarabu na kutoa udhaifu wa dai hilo.

7. Misamiati; inadaiwa kwamba kiswahili ni kiarabu katika utokeaji wa michango mbalimbali ambao waarabu walichangia ili kuweza kuhakikisha kuwa asili ya Kiswahili ni kiarabu na historia yake inajidhihirisha katika nyanja mbalimbali.

Mfano; Kiswahili : Maji.

Kisukuma; Manzi.

Kiswahili; Mtoto.

Kifipa; Umwana.

Vitenzi vya Kiswahili; pia kutokana na uwepo wa vitenzi vya kiswahili hii imepelekea kuonyesha kuwa asili ya kiswahili ni kiarabu kutokana na jina lenyewe linasadiki yale yaliyopo pia vitenzi vya Lugha hii hujidhihirisha katika namna tofautitofauti ndani ya Lugha hii ya Kiswahili.


Mfano; Cheza Chez-a, Chez-e-a-n-a.

Piga Pig-i-a, Pig-i-an-a

Zifuatazo ni sababu ambazo huonyesha udhaifu wa dai hilo kuwa Kiswahili asili yake ni kiarabu kama ifuatavyo.

Uhaba wa wataalamu hii imechangia kuwa na udhaifu mkubwa ambao utatea kuwa Kiswahili asili yake ni kiarabu kutokana na kutokuwepo kwa wataalam wa kutosha hivyo Kiswahili kushindwa kujulikana kuwa asili yake ni kiarabu kutokana na uhaba wa utaalamu unaodhihirisha dai hili.

Kasumba; pia kutokana na kuwepo kwa udhaifu huu kuwa asili ya Kiswahili ni kiarabu imepelekea kutokufahamika kuwa kiswahili asili yake ni kiarabu kutokana na kasumba ambazo zimejitokeza kwa waarabu hivyo kutokea kwa kasoro hizo.



7 Kutowahusisha wazawa wa lugha hiyo; Ingawa hii
inaonyesha kuwa asili ya Kiswahili ni Kiarabu hii
imepelekea pia kuwepo kwa udhaifu ambao unachangia
kujitetea katika maslahi tofautitofauti na kutokea
kwa udhaifu huo.
Hivyobasi Kiswahili kwa jina ni kiarabu kutokana
na mchango mkubwa ambao waliuonyesha katika kukuza
na kueneza lugha hii hivyo kupelekea Kiswahili
kujidhihirisha kuwa ni asili yake ni kiarabu. Lakini
pamoja na hivyo udhaifu wake ulijionyesha katika
nyanja mbalimbali.

Kielelezo Na. 7.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo Na.7.2, mtahiniwa alitoa hoja chache kuhusu ushahidi wa Kiswahili kuwa ni kibantu kinyume na matakwa ya swali lakini pia hakuweza kuonesha udhaifu wa hoja zenye madai kuwa Kiswahili ni Kiarabu.

### 2.1.2.4 Swali la 8: Tafsiri na Ukalimani

Swali lilihusu mada ya *Tafsiri na Ukalimani*, mada ndogo ya *Tafsiri*. Swali lililenga kupima uchambuzi na lilimtaka mtahiniwa katika kipengele (a) kuonesha tofauti tano kati ya tafsiri ya kimawasiliano na tafsiri ya kisemantiki na (b) kutafsiri sentensi (i – x) kwenda lugha ya Kiingereza kwa kuzingatia tafsiri ya kisemantiki. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote 25,050 waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa la lazima.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa, swali hili ndilo lililokuwa na ufaulu wa chini zaidi ambapo watahiniwa 11,043 sawa na asilimia 44.08 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 7 hadi 20. Jedwali Na. 3 linaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8.

**Jedwali Na. 3: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa**

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0.0 – 6.5 | 14,077 | 55.92 |
| 7.0 - 11.5 | 8,823 | 35.22 |
| 12.0 -20.0 | 2,220 | 8.86 |

Katika Jedwali Na. 3, watahiniwa 14,077 (55.92%) walipata alama hafifu 0 hadi 6.5, watahiniwa 8,823 (35.22%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 7.0 hadi 11.5 na watahiniwa 2,220 (8.86%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya nusu ya watahiniwa, (55.92%) waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama za chini kuanzia 0 hadi 6.5. Miongoni mwao, watahiniwa 907 (3.6%) walipata 0 kwa kuwa walishindwa kuonesha tofauti tano kati ya tafsiri ya kimawasiliano na tafsiri ya kisemantiki katika kipengele (a) na kutafsiri sentensi (i – x) kwenda lugha ya Kiingereza kwa kuzingatia tafsiri ya kisemantiki katika kipengele (b). Ufaulu wa chini wa watahiniwa katika swali hili ulitokana na kukosa uelewa wa mikabala mbalimbali ya tafsiri na kukosa umahiri wa kutafsiri matini kutoka lugha moja kwenda nyingine.

Katika Kujibu kipengele (a), baadhi ya watahiniwa hao walionesha kutokuelewa matakwa ya swali, hivyo kutofautisha tafsiri ya kisemantiki na ya kimawasiliano kwa kutumia vipengele vinavyotofautisha fasihi andishi na fasihi simulizi kama vile *uwasilishwaji*, *umiliki*, *gharama*, *wahusika* na *hali ya kupokea au kutopokea mabadiliko*; majibu ambayo ni kinyume kabisa na matakwa ya swali. Watahiniwa wengine walishindwa kutafsiri sentensi walizopewa katika kipengele (b) kutokana na kukosa maarifa na ujuzi wa kutumia lugha ya Kiingereza kwa ufasaha. Watahiniwa hao walifasiri kimakosa sentensi walizopewa kwa kutozingatia tafsiri ya kisemantiki kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kujibu kipengele (i) Zawadi anacheza netiboli/mpira wa pete alifasiri sentensi hiyo kama *Gift is playing net ball/ ball of ring* badala ya "Zawadi is playing netball", ambapo

alitenganisha maneno *net* na *ball*, hivyo kupotosha maana iliyokusudiwa. Vivyo hivyo, mtahiniwa mwingine katika kufasiri kipengele cha (v) Ninapendelea/ninapenda kusoma riwaya za Kiswahili aliandika, *I likeing / I like reads novel of kiswahili (*ambapo katika lugha ya Kiingereza hakuna neno likeing) badala ya "I like reading Swahili novels".

Kwa ujumla, watahiniwa hao walipaswa kuonesha tofauti tano kati ya tafsiri ya kimawasiliano na tafsiri ya kisemantiki katika kipengele (a) kama ifuatavyo:

> Tafsiri ya kisemantiki *huzingatia maana iliyotolewa na mwandishi wa lugha asilia, humtaka mfasiri afasiri kila kipengele kwa lugha asilia, haizingatii historia, utamaduni, mazingira wala itikadi ya lugha lengwa, haieleweki kwa urahisi kwa hadhira lengwa kwa kuwa haihusishi mazingira halisi na huendeleza lugha lengwa kwa sababu huingiza miundo ya lugha chanzi*, lakini Tafsiri ya kimawasiliano *huzingatia hadhira ya matini ya lugha lengwa, humpa mfasiri uwezo na uhuru wa kuongeza au kupunguza maneno ya matini ya lugha asilia, huegemea zaidi kwenye historia, utamaduni, mazingira na itikadi ya jamii lengwa, hueleweka kwa hadhira lengwa kwa kuwa huhusisha mazingira halisi, ni rahisi kuhusisha kile wanachokisoma na hali halisi katika mazingira yao na haiendelezi lugha kwa sababu hufuata sarufi ya lugha ya pili (lugha lengwa).*

Hali kadhalika katika kipengele (b), watahiniwa walitakiwa kufasiri sentensi (i – x) kwenda lugha ya Kiingereza kwa kuzingatia tafsiri ya kisemantiki kama ifuatavyo:

(i) Zawadi anacheza netiboli/mpira wa pete. (*Zawadi is playing netball*).

(ii) Mama huenda sokoni kila jumamosi/kila jumamosi mama huenda sokoni. (*Mother goes to the market every Saturday*).

(iii) Anajua chanzo cha maradhi yake/ugonjwa wake. (*He knows the source of his illness*).

(iv) Shangazi yangu/mama mdogo wangu atapika chapati tamu. (*My aunt will cook very delicious* (*''palatable'*) *chapatti*).

(v) Ninapendelea/ninapenda kusoma riwaya za Kiswahili. (I prefer reading Swahili novels).

(vi) Walimu wanafanya kazi nzuri sana. (Teachers do a very good work).


(vii) Mkutano wa wiki tatu/majuma matatu unakwisha /utakwisha /utafungwa leo. (The three weeks meeting ends today).


(viii) Kama watashinda watapewa zawadi/tuzo. (If they win they will be given a reward).

(ix) Ulisikia lakini hukutaka kujibu/kuitika. (You heard but you didn’t want to respond).

(x) Usiende, labda kama una/labda uwe na sababu ya msingi. (Don’t go, unless you have a genuine reason).

Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata alama za chini.


8. a) Tafsiri za Kimawasiliano; Ni aina
ya tafsiri ambayo hutolewa kwa-
njia ya mdomo. Wakati Tafsiri za
Semantiki; Ni aina ya tafsiri -
ambayo hutolewa kwa Maandis
hi. Zifuatazo ni tofauti kati y
a tafsiri ya kimawasiliano na
tafsiri ya Kisemantiki.
Uwasilishwaji; Hii ni kwamb
tafsiri ya Semantiki na mawasili
ano huwa tofauti kwani uwasili
shwaji wao huwa tofauti kwani
Kimawasiliano huwasilishwa kw
ai njia ya mdomo lakini kise
mantiki wa njia ya Maandishi.


8a) Tofauti katika uhifadhi: Ni kwam
ba miongoni mwa tofauti za kise
mantiki na kimawasiliano ni k
wamba mawasiliano huhifadhi
wa kichwani mara nyingi lakin
i semantiki katika Maandishi.
Tofauti katika vifaa; Hii ni k
wamba kuna tofauti kati ya
tafsiri ya kimawasiliano na -
kimantiki kwamba vifaa hutofa
utiana kwani kimantiki vifaa hi
kama kalamu, Rula, daftari lakin
hama vifaa katika Mawasiliano.
Muda; Hii ni kwamba man
tiki na Mawasiliano hutofautiar
a katika muda kwa sababu maw
asiliano hutumia muda mrefu wa
kati wa Mazungumzo kuliko tafsir
kwani ikiandaliwa husomwa haraka
haraka.
Tofauti katika kulipwa; Hii ni kw
amba kuna tofauti zilizopo kati
ya ~~Mantiki~~ na semantiki kwani
semantiki hulipwa kutokana na
Idadi ya Makaratasi yaliyoandi
kwa lakini Mawasiliano hulip
wa kutokana na Maneno
yaka alivyotoa.
8b) i/ zawadi playing netball
ii/ Mother went to market every saturd
iii/ He Is he. know source of
iv) My aunt will cook sweet chapati
v) I like to read Kiswahili play.
vi) Teachers done, good work.
vii) Meeting of three weeks shall clued today.
viii) If they are winner they given a gift
ix) you hear but didn't want to answer.
x) Don't go may be you have spec ial reason.

Kielelezo Na. 8.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 8.1, mtahiniwa alibainisha tofauti zisizo sahihi kati ya tafsiri ya kimawasiliano na semantiki akizingatia *uwasilishaji, uhifadhi, vifaa, muda na malipo* kama mambo yanayotofautisha tafsiri hizo kinyume na matakwa ya swali katika kipengele (a). Pia alitoa tafsiri isiyo sahihi katika vipengele vyote vya sehemu (b) ya swali na kupata alama hafifu.

Hata hivyo, watahiniwa 8,823 sawa na asilimia 35.22 waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 7 hadi 11.5. Watahiniwa hao walikosa umahiri katika dhana nzima ya tafsiri, hivyo walitoa majibu yasiyojitosheleza katika vipengele vingi, hususani kuonesha tofauti tano kati ya tafsiri ya kimawasiliano na tafsiri ya kisemantiki katika kipengele (a) na kutafsiri sentensi (i – x) kwenda lugha ya Kiingereza kwa kuzingatia tafsiri ya kisemantiki katika kipengele (b). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kuonesha tofauti hata moja kati ya tafsiri ya kimawasiliano na tafsiri ya kisemantiki lakini aliweza kutafsiri vipengele sita kwa usahihi na kupata alama za wastani.

Watahiniwa wachache (8.86%) tu ndio walioweza kujibu swali hili kwa usahihi na kupata alama za juu 12 hadi 20. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya tafsiri hivyo, kumudu kutofautisha ipasavyo kati ya tafsiri ya kimawasiliano na tafsiri ya kisemantiki katika kipengele (a) na kutafsiri sentensi (i – x) kwenda lugha ya kiingereza kwa kuzingatia tafsiri ya kisemantiki katika kipengele (b). Kwa ujumla, watahiniwa hao waliweza kutoa majibu sahihi katika vipengele vingi vya swali hili na kushindwa katika vipengele vichache kama Kielelezo Na. 8.2 kinavyoonesha.

8. (a) Tafsiri ya Kimawasiliano na Tafsiri ya Kisemantiki ni tafsiri au ni Miongoni katika njia nne za kutafsiri ambazo mfasiri huzitumia zaidi katika kazi yake ya tafsiri. Ambako kutokana na njia au mbinu hizi za tafsiri kuna tofauti mbalimbali ambazo huzitofautisha mbinu hizi za tafsiri nazo ni.


Tafsiri ya Kimawasiliano huegemea zaidi kwa hadhira. Ilihali, tafsiri ya Kisemantiki imeegemea zaidi kwa Mwandishi mwenyewe au Matini chanzi. Tafsiri zote hizi zina tofautiana katika utegemezi ilihali kimawasiliano huegemea zaidi hadhira inachoke gemea kutoka kwenye tafsiri lakini Tafsiri ya Kisemantiki huleta yale Mwandishi au Matini chanzi imetaka kama mfano bila kujali hadhira itaelewa kwa kiasi gani. Mfano washairi wanafasiri n.k.

Tafsiri ya Kimawasiliano inazingatia Mazingira na utamaduni wa Matini lengwa. Ilihali, tafsiri ya Kisemantiki haizingatii sana Mazingira na Tamaduni ya Matini lengwa. Mazingira na tamaduni hizo ni kama Matumizi ya Vipawe Mbalimbali, semi, Methali, vyakula, uvaaji na kadhalika.

Mfano, "like father like son" ni Matini ya Kiingereza ambayo kwa tafsiri ya - Kimawasiliano ni "Mtoto wa nyoka ni nyoka"
- Kisemantiki ni "Kama baba kama mtoto"

Katika Tafsiri ya Kimawasiliano, Mfasiri huwa huru kuchagua Maneno atakayo yatumia ili akidhi Maana ya Matini lengwa. Ilihali, tafsiri ya Kisemantiki Mfasiri hawi huru kutafsiri kwa kuchagua Maneno yake bali hufasiri Maana kama ilivyo.

Mfano, "he drink like hell" Kimawasiliano ni "amelewa kupita ndukizi" ilihali Kisemantiki "anakunywa kama kuzimu" hivyo tunaona kuna utofauti kati ya tafsiri mbili hapo juu.



8. (b) (i) Zawadi is playing netball

(ii) Mother goes at market every saturday or every saturday mother goes at market.

(iii) She/he is knowing source of his/her disease

(iv) My aunt will cook delicious chapati

(v) I like to read swahili novels

(vi) Teachers are doing better job/work

(vii) The meeting of three weeks shall end today

(viii) ~~Same~~ If they win ~~should~~ they shall awarded award

(ix) You heard but you didn't respond

(x) Donot go, May be you have important reason

Kielelezo Na. 8.2: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 8.2, mtahiniwa alitoa tofauti tano kati ya tafsiri ya kimawasiliano na tafsiri ya kisemantiki katika kipengele (a) na kufasiri sentensi saba (7) kati ya kumi alizopewa kwa usahihi katika kipengele (b), hivyo kupata alama za juu.

## 2.2 SEHEMU YA II: KISWAHILI KARATASI YA PILI

Karatasi ya pili ilikuwa imegawanyika katika sehemu A na B. Matokeo ya uchambuzi ni kama ilivyooneshwa katika sehemu zifuatazo:


### 2.2.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne yenye jumla ya alama 40, ambapo kila swali lilikuwa na alama 10. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote.

#### 2.2.1.1 Swali la 1: Fasihi kwa Ujumla

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla*, mada ndogo ya *Udhamini wa Kazi za Fasihi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza faida tatu na athari mbili za udhamini kwa mtunzi wa kazi za fasihi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (25,049) waliofanya mtihani huu. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri kwani asilimia 99.5 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kiwango cha juu kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na.7 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Katika Chati Na. 7, watahiniwa 125 (0.5%) walipata alama hafifu 0 hadi 3.0, watahiniwa 1541 (6.15%) walifaulu kwa kiwango cha

wastani kwa kupata alama 3.5 hadi 5.5 na watahiniwa 23,383. (93.35%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 6 hadi 10.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 23,383 sawa na asilimia 93.35, walijibu vizuri swali hili na kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Miongoni mwao, watahiniwa 11,205, sawa na asilimia 44.7, walifanya vizuri zaidi na kupata alama za juu kuanzia 8 hadi 10. Ufaulu wao ulitokana na kuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ndogo ya *Udhamini wa Kazi za Kifasihi*. Uchambuzi unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa waliweza kueleza kwa usahihi faida tatu za udhamini kama vile; *kugharamia utafiti wa kazi ya fasihi ili ziwe bora, husaidia kuwepo kwa maendeleo ya kazi za fasihi nchini, husaidia kutoa ajira kwa watunzi na husababisha ongezeko kubwa la wataalamu wa kutunga kazi za fasihi.* Pia, waliweza kueleza athari mbili za udhamini kwa mtunzi wa kazi za fasihi kama vile; *kukosa uhuru wa kutunga kutokana na ushawishi wa fedha ili kukidhi matakwa ya mdhamini, hushindwa kukemea mambo yanayotokea katika jamii kutokana na mwelekeo wa mdhamini*, *husababisha kazi ya fasihi kuwa mali ya mdhamini, hivyo kumnyima mtunzi haki yake ya umiliki* na *huweza kutunga kazi za aina moja tu* (*pendwa*). Aidha, baadhi ya watahiniwa walitoa hoja pungufu lakini walizitetea kikamilifu na kupata alama za juu. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.


1. Udhamini.- Ni hali ya kutoa pesa au kitu chochote cha thamani ili kugharamia kazi ya kifasihi. Ndio ni kweli Udhamini unaweza kuleta faida na hasara pia.

FAIDA ZA UDHAMINI

=> Kuibua vipaji mbalimbali katika soko la sanaa. pale ambapo msanii anapodhaminiwa hupelekea kuibua kwa vipaji ambavyo vilijificha kutokana na kukosa pesa. mfano Udhamini wa Abdul Na sib (Diamond) kwa Zuchu umepelekea kuibua ki paji chake.

=> Kuleta ushindani katika utunzi wa kazi za kifasihi, Wasanii wanapodhaminiwa huwafanya washindane katika tasnia ya sanaa na kupelekea kuongezeka kwa kazi za kifasihi

=> Kusaidia msanii au mtunzi kujipatia fedha. msanii anapodhaminiwa kazi humsaidia kujipatia fedha kwani kazi hiyo inakuwa imeandaliwa vizuri na kuchapwa na kutafutiwa masoko. mfano, aliyedhaminiwa (Rayvany) Raymond inamsaidia kujipatia pesa

ATHARI

=> Kupelekea kazi ya msanii kumilikiwa na md hamini ambaye ametoa gharama zake kudhamini kazi hiyo, hivyo kusababisha mtunzi akiwa hana mamlaka makubwa juu ya kazi hiyo

=> husababisha wasanii wengi kupenda pesa kulo kazi ya kuelimisha jamii, msanii anapodhaminiwa huwapelekea wao kupenda sana fedha na kusahau kazi yao ya kuelimisha jamii.

Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 9.1, mtahiniwa alielezea kwa usahihi faida tatu na athari mbili za mdhamini kwa mtunzi wa kazi za fasihi japokuwa hakutoa ufafanuzi wa kutosha katika mifano aliyoitumia.

Vilevile, uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 1,541 sawa na asilimia 6.15 walijibu swali hili na kupata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5. Watahiniwa hao walishindwa kuelezea kikamilifu faida na athari za udhamini kwa mtunzi wa fasihi, wengine walichanganya hoja zinazohusu faida na zile zenye athari ya udhamini kwa mtunzi wa kazi za fasihi. Katika kundi hili, wapo watahiniwa ambao hawakuandika utangulizi wala hitimisho katika majibu yao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza faida tatu kama vile *kukuza vipaji vya uandishi, kuelimisha jamii na kutetea/kulinda maslahi ya mdhamini* ambapo, hoja mbili zilikuwa sahihi lakini ufafanuzi wake haukujitosheleza, na hoja ya tatu ilihusu athari za udhamini wa kazi za fasihi, hivyo haikuwa sahihi.

Pia, uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa watahiniwa wachache, (125) sawa na asilimia 0.5 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3. Tathmini ya majibu ya watahiniwa wa kundi hili inaonesha kuwa watahiniwa wengi hawakuelewa matakwa ya swali kwani baadhi yao walieleza faida na athari za *mhakiki* wa kazi ya fasihi kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha faida ya udhamini kwa mhakiki kama vile: *humsaidia kutoa tahakiki sahihi, humsaidia mhakiki kuzingatia vipengele vya fani na maudhui katika tahakiki yake* na *humsaidia mhakiki kuwa huru na kazi na kutoa tahakiki bila ya upendeleo*. Kadhalika, watahiniwa wengine walielezea faida/athari chache za udhamini kwa mtunzi wa kazi za fasihi lakini walishindwa pia kutoa mifano ili kufafanua hoja hizo, hivyo kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

1 Fasihi ni kazi moja muhimu sana
inayomfanya mtaalamu wa lugha
kuweza kufurahi na kupenda kazi
yake na kuifanya ipasavyo.
Zifuatazo ni faida za udhamini
kwanza: Kazi hii ni huru. Pamoja na kazi
hii kuwa huru sio lazima kupata udhamini
maana kazi ya fasihi ni mtu mwenye
we anaeifanya kazi huyo.
Pili. Inawahusu watu wachache.
kazi ya fasihi haina mlolongo mwingi
wa washiriki hivyo ni kazi rahisi
sana kuweza kuimudu.
Tatu Imesambaa maeneo mengi.
Kwakuwa kazi hii ni maarufu haina
uhitaji sana wa udhamini kwani
inajulikana na kuheshimika
Kila jambo likiwa na faida
halikosi hasara hizi ni athari za
udhamini kwa mtunzi wa kazi za fasihi.
Kwanza udhamini ni muhimu
kwani kazi yoyote kubwa na maarufu
ni lazima iwe na udhamini bila
udhamini siku moja shida inaweza kuja.
Mwisho maisha ya kazi
hayakosi changamoto. Hivyo hata kazi
zetu hazikosi faida na hasara.


Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 9.2, mtahiniwa alielezea faida za udhamini kwa mtunzi wa kazi ya fasihi kinyume na matakwa ya swali hili.

### 2.2.1.2 Swali la 2: Maendeleo ya Fasihi Simulizi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Fasihi Simulizi*, katika mada ndogo ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Simulizi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kutathmini umuhimu wa michezo ya watoto kama utanzu mmojawapo wa sanaa za maonyesho.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (25,049) waliofanya mtihani huu. Ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri sana, ambapo watahiniwa 24,624, sawa na asilimia 98.30, walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kiwango cha juu kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*

Katika Chati Na. 8, watahiniwa 425 (1.70%) walipata alama hafifu 0 hadi 3.0, watahiniwa 2,389 (9.54%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3.5 hadi 5.5 na watahiniwa 22,235 (88.77%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 6 hadi 10.

Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili walikuwa 22,235 sawa na asilimia 88.77 ambapo walipata alama kuanzia 6 hadi 10. Miongoni mwa watahiniwa waliofanya vizuri, asilimia 30.1 walitoa majibu sahihi na kupata alama za juu 8.5 hadi 10. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ndogo ya uhakiki wa kazi za fasihi simulizi hasa katika utanzu wa sanaa za maonesho, hivyo kueleza kwa usahihi umuhimu wa michezo ya watoto kama utanzu mmojawapo wa sanaa za maonyesho. Watahiniwa hao waliweza kutumia hoja tano

sahihi na mifano katika kutathmini umuhimu wa michezo ya watoto kama vile: *kukuza ujasiri, ushujaa na udadisi wa jambo, kukuza umoja na ushirikiano miongoni mwa watoto, kujenga/kuboresha afya za watoto, kukuza na kuibua vipaji vya* watoto, *kuwafanya watoto kujitambua na kutambua majukumu yao ya baadaye*, *kukuza uwezo wa kujifunza, kujua lugha* na *kuburudisha watoto kupitia michezo mbalimbali.* Kielelezo Na.10.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.




02. Michezo ya Watoto; Huu ni utanzu mmojawapo wa sanaa za maonyesho ambao huonyeshwa ~~faid~~ na watoto katika jamii. Michezo ya watoto hujumuisha nyimbo, sarakasi, zifuatazo ni umuhimu wa michezo ya watoto.

Hukuza udadisi wa jambo. Kupitia michezo ya watoto huchochea udadisi miongoni mwao kwani kupitia michezo hiyo watoto watataka kufahamu mambo mbalimbali yaliyoweza kutokea katika jamii kwa undani zaidi.

Hukuza umoja na ushirikiano miongoni mwa watoto. Pia kupitia michezo ya watoto hupelekea umoja na ushirikiano miongoni mwa watoto kwani kila mmoja wanaona kuwa ni ndugu wa familia moja hivyo basi hata kupigana ovyo hawataweza kupigana tena.

Huboresha afya za watoto. Pia kupitia michezo ya watoto afya zao zitaweza kuboreka kwani watoto huwa na mazoea ya kukimbia kimbia hivyo basi hata magonjwa kama kisukari na hata magonjwa mengine hayataweza kushambulia kiurahisi.

Hukuza vipaji vya watoto. Pia kupitia michezo ya watoto miongoni mwao wataweza kuonyesha vitu gani walivyojaaliwa navyo ambavyo ni vya tofauti kabisa na watoto wenzao katika jamii hivyo basi kupitia michezo ya watoto vipaji




02. vya watoto kukua.
Huwafunza watoto majukumu
yao ya baadaye. Pia kupitia Michezo
ya watoto huweza kuwaandaa wato-
to katika kupambana na Maisha yao
ya baadaye hata wakiwa ni watu
wazima, kupitia Michezo ya watoto huw
afunza watoto hao maisha ya watu
Wazima kama vile kuwapeleka watoto wao
shule, kuwapulia watoto wao pamoja na
kuwapeleka Hospitalini kwaajili ya Matibabu
Kwa kuhitimisha: Tunaona ya kuwa
Michezo ya watoto pia huwa na
athari zake katika jamii kwampano
huwababisha Vifo pia hata huwaba-
bisha Mmomonyoko wa Maadili katika
jamii.

Kielelezo Na. 10.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 2,389 (9.54%) waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5. Katika kujibu swali hili, baadhi ya watahiniwa walirudia hoja hivyo kuwa na hoja chache, wengine walitoa hoja bila ufafanuzi unaojitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea umuhimu wa michezo ya watoto kama vile kuwa *mcheshi, mchangamfu, mkarimu, jasiri* na *mwenye akili timamu;* hoja ambazo kiuhalisia zinamjenga mtoto kimwelekeo zaidi kuliko kivitendo, hivyo alipata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (1.70%) waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3. Miongoni mwa sababu zilizoathiri ufaulu wa watahiniwa katika kundi hili ni kukosa umahiri kuhusu michezo ya watoto kama utanzu mmojawapo wa sanaa za maonyesho. Uchambuzi umebaini kuwa baadhi ya watahiniwa walijadili michezo mbalimbali inayofanywa na watoto kama vile *mdako*, *rede*, *kuruka kamba*, *kukimbiza kuku* na mingineyo. Aidha, wengine walielezea sifa za michezo ya watoto kama vile: *yenye kuibua vipaji*, *isiyoumiza*, *inayotendwa kwa urahisi* na *inayotendeka* badala ya kueleza umuhimu wa michezo ya watoto kama utanzu mmojawapo wa sanaa za maonyesho kama vile; *kukuza ujasiri*, *ushujaa na udadisi wa jambo, kukuza umoja na ushirikiano miongoni mwa watoto,*

*kujenga/kuboresha afya za watoto, kukuza na kuibua vipaji vya* watoto, *kuwafanya watoto kujitambua na kutambua majukumu yao ya baadae*, *kukuza uwezo wa kujifunza lugha* na *kuburudisha watoto kupitia michezo mbalimbali.* Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali, hivyo kupata alama hafifu.



2 Sanaa za maonyesho ni sanaa ambayo inatumika mbele ya hadhira ambapo ni fanani na hadhira huonana. Sanaa hii inaweza kufanyika kokote kule ambapo patakuwepo na hadhira. Zifuatazo ni umuhimu wa michezo ya watoto katika kutathmini kama sanaa za maonyesho.

Jukwaa, ni sehemu ambayo sanaa hiyo itakapofanyikia; watoto wanaweza kucheza au kufurahi jukwaani kwa michezo tofauti.

Kutathmini hadhira waliopo, vilevile ni muhimu kuwepo na hadhira ambapo wataangalia watoto hao wanapocheza kwa kuburudika kwa hadhira na watoto vilevile.

Mahali pa kuchezea, au sehemu ya maonyesho inawezekana kuwa uwanjani, shuleni, sokoni na mtaani. Ni sehemu yeyote au maalum ambapo maonyesho hayo kufanyika.

Sehemu ya kukaa, kwa wahusika, hadhira huwaeleka waliopo jukwaani ~~kwani~~ ili kuangalia michezo hiyo. Sehemu za kukaa hadhira ni tofauti wanapokaa wahusika wa sanaa hiyo mfano watoto ni watakaa nyuma ya jukwaa kwasababu ndio walengwa.

Kutathmini mbinu ya kisanaa kimaudhui au kifani ~~yaa~~ je inafundisha? Kazi yeyote ya kisanaa au kifani lazima ifundishe mfano Michezo ya watoto inafundisha. mfano kwa kuimba.

Hivyobasi sanaa za maonyesho inathamani kubwa kwani huleta ujumbe kwa hadhira wote kwani huelimisha huburudisha. na kukuza kwa sanaa hiyo.

Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi ya swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 10.2 Mtahiniwa aliyeeleza baadhi ya sifa za fasihi simulizi kama vile *jukwaa, hadhira* na *mbinu za kisanaa* kinyume na matakwa ya swali.

#### 2.2.1.3 Swali la 3: Maendeleo ya Fasihi Simulizi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Fasihi Simulizi*, katika mada ndogo ya *Kuhakiki Kazi za Fasihi Simulizi*. Swali lilimtaka mtahiniwa aoneshe namna vipengele vya muundo, mtindo, sitiari, tashihisi na taswira vinavyojibainisha katika vitendawili.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa swali hili lilijibiwa vizuri na lilifanywa na watahiniwa 20,049, sawa na asilimia 100. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 16,056 sawa na asilimia 64.10, walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kiwango cha juu zaidi kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Jedwali Na. 4 linaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3.


**Jedwali Na. 4: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa**

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0.0 – 3.0 | 8,993 | 35.90 |
| 3.5 - 5.5 | 6,711 | 26.79 |
| 6.0 -10.0 | 9,345 | 37.31 |

Katika Jedwali Na. 4, watahiniwa 8,993 (35.90%) walipata alama hafifu 0 hadi 3.0, watahiniwa 6,711 (26.79%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3.5 hadi 5.5 na watahiniwa 9,345 (37.31%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6 hadi 10.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 9,345, sawa na asilimia 37.31, walifaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Kati yao, watahiniwa 2,939, sawa na asilimia 11.7, walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10. Watahiniwa hao waliweza kuonesha namna vipengele vya muundo, mtindo, sitiari, tashihisi na taswira vinavyojibainisha katika vitendawili. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili waliweza kuonesha kwa usahihi namna kila kipengele kinavyojibainisha kwenye vitendawili. Majibu ya mtahiniwa mmojawapo yanavyodhihirisha kama vile; *muundo;* utangulizi, kitendawili chenyewe, swali la msaada, mji na jibu; *Mtindo*-(majibizano), *sitiari* huunganisha vitu viwili tofauti bila kutumia kiunganishi mfano, uzi mwembamba, unamfunga dume mkubwa,


*tashihisi* hukipa kitu kisicho na uhai sifa ya uhai mfano, kila niendako ananifuata – kivuli, ambapo kivuli kinapewa sifa ya kutenda kama kiumbe hai, na *taswira* mfano, blanketi la babu lina chawa, ambapo blanketi ni taswira ya mbingu na chawa ni taswira ya nyota. Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.


8. i/ Muundo
Katika vitendawili muundo huweza kujibainisha kutokana na mpangilio wa kitendawili chenyewe. Maranyingi vitendawili huwa na muundo wa, mwanzo, kati na mwisho.
Kwa mfano: Mtambaji : Kitendawili . . . . .
Hadhira : Tega
Mtambaji : Popoo mbili zavuka mto
Hadhira : Macho.

ii/ Mtindo
Katika vitendawili kuna mtindo wa dayolojia ambapo mtegaji na mteguaji hujibizana mpaka jibu la kitendawili linapopatikana.
Kwa mfano: Mtegaji :- Kitendawili
Mteguaji : Tega
Mtegaji : Nyumba yangu haina mlango
Mteguaji : Yai

iii/ Sitiari
Katika vitendawili baadhi huweza kuwa na ulinganishi wa dhana mbili tofauti bila kutumia viunganishi
Kwa mfano Mtegaji : Pala la babu linafuka moshi
Jibu : Ugali.

iv/ Tashihisi
Baadhi ya vitendawili vinavipa sifa za binadamu vitu visivyo binadamu. Kwa mfano "Popoo mbili zavuka mto" kwamba Popoo


8. Wamekuwa na uwezo wa kuuka mto kama binadamu.

v/ Taswira
Baadhi ya vitendawili vinakuwa na taswira ndani yake.
Kwa mfano: Kuku wangu hutagia miibani - Nanasi.

Kielelezo Na.11.1: Sampuli ya jibu sahihi ya swali la 3.

Kadhalika, watahiniwa 6,711, sawa na asilimia 26.79, walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5. Kulingana na uchambuzi baadhi yao waliweza kueleza kwa usahihi namna vipengele vya muundo, mtindo, sitiari, tashihisi na taswira vinavyojibainisha katika vitendawili lakini mifano waliyoitoa ilikuwa haiendani na utendekaji wa vitendawili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kwa usahihi namna tashihisi inavyojibainisha katika vitendawili lakini alitoa mfano wa methali kama vile “wajinga ndio waliwao.” Kwa ujumla, watahiniwa hao walionesha kuelewa matakwa ya swali lakini hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya fani ya vitendawili.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 8,993, sawa na asilimia 35.90, walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3. Sababu za ufaulu huo ni pamoja na watahiniwa kutoa majibu yasiyojitosheleza katika kuonesha namna vipengele vya *muundo, mtindo, sitiari, tashihisi* na *taswira* vinavyojibainisha katika vitendawili. Baadhi ya watahiniwa walionesha kukosa maarifa kuhusu vipengele vya fani katika vitendawili ambapo walielezea vipengele hivyo katika kazi za riwaya, tamthiliya na ushairi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha mtindo wa masimulizi katika tamthiliya ya “Nguzo Mama” kinyume na matakwa ya swali. Watahiniwa wengine walikuwa na uelewa mdogo juu ya vipengele vya *muundo, mtindo, sitiari, tashihisi* na *taswira* ambapo walitoa majibu kama vile; *vitendawili hutumia lugha, vitendawili hutumia taswira, vitendawili hutumia tamathali za semi, vitendawili hutoa funzo* na *vitendawili vina mafumbo.* Majibu yasiyo sahihi kwa alitakiwa kuonesha namna vipengele hivyo

vinavyojibainisha katika vitendawili. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali la 3.

3. Vitendawili ni utanzu wa fasihi simulizi ambao hupima fikra za hadhira na uelewa. Vipengele vya muundo, mtindo, sitiari, tashihisi na taswira hujibainisha katika vitendawili kama ifuatavyo:-


Muundo; Ni mpangilio wa visa na matukio katika vitendawili ~~msanii~~ fanani anatakiwa kupangilia visa na matukio yake ili kuleta ujumbe kwa hadhira.

Mtindo; ni mbinu anazotumia katika vitendawili, hivyo fanani anatakiwa atumie mbinu mbalimbali kwa ajili ya kunasa makini ya hadhira wake.

Sitiari; ni tamathali ya semi ambayo hulinganisha vitu bila kutumia ~~ma~~ viunganishi mfano Dunia jiti kavu na mke ni nguo mkomba kupaliliwa. sitiari hutumika katika vitendawili kwa ajili ya kutoa radha ambayo itawavutia hadhira.

Tashihisi; Hii ni tamathali ya semi ambayo huvimba vitu sifa za kutenda kama binadamu vitu ambavyo havina sifa za binadamu. Mfano rushwa kajenga kambi, siri ya mtungi ajuaye kata na kunguru wakawa ni wezi. tamathali hii ya semi hutumika katika vitendawili kwa ajili ya kuwavutia hadhira.

Taswira; ni picha ambayo hujengeka akilini mwa mtu au hadhira baada ya kusoma au kusikiliza kazi ya fasihi. mfano paka ikiaph via wizi. taswira hutumika katika vitendawili kwa ajili ya kukosoa jamii kwa njia isiyo ya moja kwa moja.



| | |
|---|---|
| 3. | Kwa ujumla vitendawili vinadhima mbali |
| | mbali katika jamii kama vile kuelimisha jamii, |
| | kuburudisha, kukosao na kuonya jamii na |
| | kukuza na kuendeleza lugha. |

Kielelezo Na. 11.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3.

Katika Kielelezo Na.11.2 mtahiniwa alielezea umuhimu wa kutumia muundo na mtindo katika vitendawili lakini alitumia mifano ya methali kinyume na mahitaji ya swali.

### 2.2.1.4 Swali la 4: Usanifu wa Maandishi

Swali hili lilikuwa mahsusi kupima uchambuzi na lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *Usanifu wa Maandishi.* Swali lilimtaka mtahiniwa kusoma matini ya ushairi kisha kubainisha vipengele vyake vya kifani.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 25,049, ambapo watahiniwa 13,414 sawa na asilimia 53.55 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kiwango cha juu zaidi kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Jedwali Na. 5 linaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali.

**Jedwali Na. 5: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa**

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0.0 – 3.0 | 11,634 | 46.45 |
| 3.5 - 5.5 | 9,843 | 39.30 |
| 6.0 -10.0 | 3,571 | 14.26 |

Katika Jedwali Na. 5, watahiniwa 11,634 (46.45%) walipata alama hafifu 0 hadi 3.0, watahiniwa 9,843 (39.30%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3.5 hadi 5.5 na watahiniwa 3,571 (14,26%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6 hadi 10.

Licha ya swali hili kuwa na ufaulu wa wastani, uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa watahiniwa 11,634, sawa na asilimia 46.45, walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama 0 hadi 3. Miongoni mwao,

watahiniwa 373, sawa na asilimia 1.5, walipata alama 0. Watahiniwa hao walionesha kukosa uelewa kuhusu usanifu wa maandishi, hivyo kushindwa kubainisha vipengele mbalimbali vya kifani vilivyojitokeza katika shairi walilopewa. Baadhi yao walinukuu baadhi ya mistari kutoka katika beti za shairi bila kutoa ufafanuzi wowote. Wengine walijadili vipengele vya kimaudhui kama vile dhamira mbalimbali zinazojitokeza katika beti za shairi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alionesha dhamira ya *umaskini* katika ubeti wa kwanza, *matabaka* katika ubeti wa pili, *rushwa* katika ubeti wa nne na *uongozi mbaya* katika ubeti wa tano; majibu ambayo hayahusiani na vipengele husika vya kifani vya shairi hili.

Kiuhalisia, mtahiniwa alitakiwa kusoma shairi kisha kubainisha vipengele vya kifani kama ifuatavyo: muundo wa shairi (tarbia) mtindo (masimulizi ya nafsi ya tatu umoja), wahusika (Mwanambuzi), mandhari (nchi za kiafrika) na matumizi ya lugha yaliyosheheni tamathali za semi kama vile sitiari (mwanambuzi kawa pambo) na taswira (Mwanambuzi) ya mnyonge mwenye maisha ya dhiki, anayeonewa, kudharauliwa na taswira ya "kamba na fimbo" zinazotoa picha ya matatizo na shida zinazomnyima mwanadamu uhuru. Aidha, mtunzi alitumia lugha ya mkato (lugha ya kishairi) kama vile "ha'shiwi" akimaanisha haishiwi na “hubembezwa” akimaanisha hubembelezwa. Kielelezo Na. 12.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyokidhi matakwa ya swali.

4. Soma shairi lifuatalo kisha bainisha vipengele vyake kifani:

i/ MAUDHUI

Dhamira

a) Umasikini katika ubeti wa pili

b/ Malabaka katika ubeti wa pili

c/ Rushwa ubeti wa nne

d) Uongozi mbaya ubeti, wa tano

e/ Kufanya mapinduzi

ii/ Ujumbe

a/ ukoloni mambo leo ni kikwazo kwa jamii yetu

b/ Mageuzi yanatakiwa ili kuweza kuleta maendeleo kwa jamii

c/ Rushwa ni adui wa haki

iii FALSAFA

Falsafa ya mwandishi ni kwamba watu wanapata mateso kutokana na uongozi mbaya.


iv/ MTAZAMO

Mwandishi anamtazamo wa kimapinduzi kwa jamii

Kielelezo Na. 12.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi ya swali la 4.

Takwimu zinaonesha kuwa, watahiniwa 9,843, sawa na asilimia 39.30 ya waliofanya mtihani walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5. Watahiniwa hao walifafanua kwa usahihi baadhi ya vipengele vya kifani huku wakishindwa vingine. Aidha, baadhi yao walichanganya vipengele vya fani na vipengele vya maudhui mfano waliandika vipengele vya maudhui kama, *ujumbe, dhamira* na *falsafa* katika majibu yao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua kwa usahihi vipengele kama vile: *wahusika, mandhari, matumizi ya taswira, mtindo na muundo*; lakini alishindwa kutoa mifano sahihi kwa baadhi ya vipengele, hivyo akapata alama za wastani.

Licha ya swali hili kuwa na ufaulu wa chini, baadhi ya watahiniwa (asilimia 14.26) walifaulu vizuri na kupata alama za juu kuanzia 6 hadi 10. Miongoni mwao, watahiniwa wachache, (2.1%) walipata alama kuanzia 8 hadi 10 kwa kuwa waliweza kubainisha kwa usahihi vipengele vyote vya kifani katika shairi walilopewa. Watahiniwa hao walibaini kwa usahihi vipengele vifuatavyo; muundo *wa shairi* (*tarbia*), mtindo (*nafsi/masimulizi*), wahusika (*Mwanambuzi*), mandhari (*nchi za Afrika*), matumizi ya lugha na tamathali za semi kama *sitiari*, na *taswira.* Aidha, katika kubainisha vipengele hivyo, alitoa mifano sahihi kutoka kwenye shairi walilopewa. Kielelezo Na.12.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kukidhi matakwa ya swali.



4

Kubainisha vipengele vya fani.

A. MUUNDO


Muundo uliotumika katika shairi hili ni muundo wa tarbia ambapo, kila ubeti una mshororo minne.

- Shairi lina vipande viwili kwa kila mshororo
Mfano, "Maisha ya mwanambuzi/si leo tangu kitambo
Utao Ukwapi

- Katika shairi hili kuna idadi sawa ya mizani yani kila mshororo una mizani kumi na sita
Mfano,
"Mbele kamba nyuma fimbo, maisha ya mwanambuzi
1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16

B. MTINDO

-Mtindo uliotumika ni mtindo wa kiitikio, ambapo, mshoroto wa mwisho umejirudia katika beti zoto, na mshororo ~~huo~~ huo ni
"Mbele kamba nyuma fimbo, maisha ya mwanambuzi."



4 - Mtindo wa masimulizi; Maisha ya mwanambuzi yamesimuliwa kuanzia mwanzo hadi mwisho kuwa Mwanambuzi yana onekana ni ya kinyonge.

- Matumizi ya nafsi
Mfano; Yapekue mpekuzi maisha yale ni chambo
Nafsi ya II umoja.

- Mtindo wa takriri; ambapo maneno "mwanambuzi" limerudiwa katika kila beti.

C. WAHUSIKA.

i> Mwanambuzi - Mnyonge

ii> Mpekuzi - Mtu anayepanga utafiti

(iii) Mchunga - Anayelinda na kulisha mifugo

D. MANDHARI.

i> Porini - kuchunga mbuzi wapate malisho.

ii> Nyumbani - Mbuzi hufugiwa nyumbani kama mapambo

E. MATUMIZI YA LUGHA.

i> Msemo
Mfano; Mbele kamba nyuma fimbo

ii> Sitiari
Mfano; Ni maisha ya gubizi, tena yananuka shombo

iii> Maneno yenye ukinzani
Mfano; Mbele kamba nyuma fimbo

(iv) Taswira
Mfano; Mwanambuzi - tabaka tawaliwa.

Kielelezo Na.12.2: Sampuli ya jibu sahihi ya swali 4.

Katika Kielelezo Na.12.2, mtahiniwa alibainisha kwa usahihi vipengele vya kifani katika shairi lakini alishindwa kutoa mifano sahihi ya sitiari na taswira zilizotumika katika kifungu cha ushairi.


### 2.2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAREFU

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) ya insha ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu. Swali la tano lilikuwa ni la lazima. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 60, ambapo kila swali lilikuwa na alama 20.

#### 2.2.2.1 Swali la 5: Uhakiki wa Ushairi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia diwani mbili alizosoma na kutoa hoja tatu na mifano kwa kila diwani kutetea hoja kuwa, “Mtunzi bora ni yule anayebainisha mikakati ya kukabili changamoto mbalimbali katika jamii.”

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (25,049) waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri sana ambapo watahiniwa 24,975 sawa na asilimia 99.70 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kiwango cha juu kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 20. Chati Na. 9 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 5.




**Chati Na. 9**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Katika Chati Na. 9, watahiniwa 74 (0.30%) walipata alama hafifu 0 hadi 6.5, watahiniwa 970 (3.87%) walifaulu kwa kiwango cha wastani

kwa kupata alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 24,005 (95.83%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa watahiniwa 24,005 sawa na asilimia 95.83 walijibu vizuri na kupata alama kuanzia 12 hadi 20. Miongoni mwao, watahiniwa 2,596 sawa na asilimia 10.4 walifaulu kwa kiwango kizuri zaidi na kupata alama za juu kuanzia 18 hadi 20. Ufaulu mzuri wa watahiniwa ulitokana na kuweza kutambua na kukidhi matakwa ya swali ipasavyo pamoja na kuwa na uelewa wa kutosha wa diwani teule. Watahiniwa hao waliweza kutumia mifano mitatu kutoka katika diwani mbili walizosoma kutetea hoja kuwa *Mtunzi bora ni yule anayebainisha mikakati ya kukabili changamoto mbalimbali katika jamii*. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa na watahiniwa hao ili kukabili changamoto mbalimbali katika jamii zilizobainishwa na watunzi wa diwani teule ni kama vile; "Chungu Tamu" - *kujitoa mhanga, kupinga suala la matabaka na ubaguzi wa rangi* na *kupinga uongozi mbaya.* Katika diwani ya "Fungate ya Uhuru", walibainisha mikakati ya kukabili changamoto ya uzalendo, *kupiga vita rushwa, kupinga ukoloni mkongwe* na *ukoloni mamboleo.* Aidha, watahiniwa hao walitumia mifano sahihi ya mashairi yanayopatikana katika diwani hizo yenye dhima ya kuonesha changamoto hizo. Kwa mfano, "Chungu Tamu" katika mashairi kama: *Naipenda Nchi Yangu, Viongozi wa Afrika* na *Nikizipata Bunduki,* ambapo katika "Fungate ya Uhuru" alielezea changamoto ya kukosekana mapenzi ya dhati katika jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kujibu kwa usahihi swali hili na kupata alama za juu ambapo katika diwani ya "Chungu Tamu" alibainisha mikakati kama; *kupiga vita usaliti, matabaka* na *uvivu* ambapo aliweza kutoa pia mifano dhahiri ya mashairi kutoka katika diwani teule. Pia, alikuwa na utangulizi na hitimisho zuri linaloendana na swali. Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.


5 Mikakati ya kukabili changamoto, ni mipango mbalimbali inayopangwa ili kuweza kukabili matatizo mbalimbali katika jamii. Mtunzi bora ni yule anayeweza kubainisha mikakati ya kukabili changamoto mbalimbali katika jamii. Katika diwani watunzi wameweza kubainisha mikakati hiyo. Katika diwani ya CHUNGU TAMU iliyoandikwa na THEOBALD MVUNGI pamoja na diwani ya FUNGATE YA UHURU iliyoandikwa na MOHAMED S. KHATIBU, watunzi wamefanikiwa kubainisha mikakati ya kukabili changamoto mbalimbali katika jamii. Kwa kuanza na diwani ya FUNGATE YA UHURU, zifuatazo ni mikakati ya mtunzi katika kukabili changamoto za jamii.

Kupiga vita wizi katika jamii, mtunzi wa diwani amebainisha mkakati wa kupiga vita suala zima la wizi katika jamii za kiafrika. Katika shairi la "Kunguru" mtunzi anasema.

"Kunguru wakawa ni wezi,
Kuiba hawana ajizi,
Chochote wakipimaizi,
Hawaufichi ujambazi".

Mtunzi anaeleza jamii za kiafrika zimejaa wizi hivyo ni lazima kupiga vita suala hilo ili kuweza kukabili changamoto hii.

Kupiga vita suala la usaliti katika jamii, pia mtunzi wa diwani anaonesha suala la usaliti katika jamii linavyoathili maisha ya watu katika jamii. Hivyo anaamua kupanga mkakati wa kukabili changamoto ya usaliti katika jamii yake. Katika shairi la "Si Wewe?" mtunzi wa diwani anaonesha usaliti.



5 "Si Wewe?
Ulinijia mapema kama ukiwa yatima,
Nikawa kama wako baba na mama,
Kakuendesha tata,
Si wewe uso hisani".

Katika jamii za kiafrika watu wengi ni wasaliti. Viongozi huwasaliti wananchi lakini pia wanandoa husalitiana. Mtunzi anaitaka jamii ipige vita suala la usaliti katika jamii.

Kupiga vita suala la matabaka, mtunzi wa diwani anabainisha mkakati wa kukabili changamoto katika jamii kwa kupiga vita suala zima la matabaka katika jamii. Jamii nyingi zina matabaka kati ya maskini na matajiri, wenyenavyo na wasiokuwa navyo pamoja na walujumu uchumi na wapiganaia haki. Katika shairi la "Nataka kusema" mtunzi anaeleza.

"Nataka kusema yote,
Yote yaniumizayo moyo,
Lakini nna kitata,
Siwezi kutamka"

Katika jamii za kiafrika swala la matabaka ni jambo ambalo kwalo haliepukiki. Mtunzi anaiomba jamii ishirikiane katika kupiga vita matabaka kwenye jamii za kiafrika.

Kielelezo Na. 13.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5.

Pamoja na ufaulu mzuri wa watahiniwa, baadhi ya watahiniwa (asilimia 3.87) walikuwa na ufaulu wa wastani kwani walipata alama 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza katika kutetea hoja kuwa, *mtunzi bora ni yule anayebainisha mikakati ya kukabili changamoto mbalimbali katika jamii*. Baadhi ya watahiniwa walitoa dhima sahihi za ushairi lakini wakashindwa kutetea baadhi ya hoja zao

kikamilifu, wengine walitaja hoja pungufu lakini sahihi kulingana na diwani walizosoma. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika diwani ya "Fungate ya Uhuru" alibainisha changamoto zifuatazo: *kuadibu jamii, kutia hamasa jamii na kuhifadhi mila* na *desturi za jamii, hoja ambazo kiuhalisia ni mikakati ya kukabili changamoto mbalimbali katika jamii.* Katika diwani ya "Mapenzi Bora" alitoa dhima kama vile: *aina za mapenzi bora, sifa za mapenzi bora* na *faida za mapenzi bora* na kuzielezea kwa kina. Majibu hayo yanaonesha kuwa mtahiniwa huyo alishindwa kutofautisha dhana ya changamoto na mikakati, hivyo majibu yalikuwa na mapungufu na kusababisha kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 74, sawa na asilimia 0.30 walikuwa na ufaulu hafifu ambapo walipata alama kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kushindwa kutetea hoja kuwa *mtunzi bora ni yule anayebainisha mikakati ya kukabili changamoto mbalimbali katika jamii*. Watahiniwa hao walionesha kukosa uelewa wa mashairi mbalimbali yaliyopo katika diwani teule ambapo baadhi ya watahiniwa walijadili vipengele vya fani badala ya kutetea hoja. Wengine walieleza hoja kama; *matumizi ya taswira, matumizi ya misemo, matumizi ya lugha ya mafumbo, matumizi ya mandhari na matumizi ya mafumbo, m*ajibu ambayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yasiyo sahihi katika diwani ya "Kimbunga" kama vile; *tabaka tawala kuwasikiliza tabaka tawaliwa, usawa katika jamii na kupinga na kukataa rushwa*, hoja ambazo ufafanuzi wake haukuwa sahihi. Pia, alitumia diwani moja tu badala ya mbili kama swali lilivyomtaka na alishindwa kuthibitisha kwa mifano sahihi juu ya mikakati husika toka katika diwani teule. Kielelezo Na.13.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kupata alama hafifu.

5. Ujumbe hili ni lengo ~~ku~~ la msanii tunalolipata katika kazi ya fasihi. Msanii hutunga kazi yenye ujumbe ili kuweka mikakati ya kukabili changamoto mbali mbali. Kwa kutumia diwani ya KIMBUNGA iliyoandikwa na HAJI GORA na FUNGATE YA UHURU iliyoandikwa na MOHAMED S. KHATIBU.

Kwa kuanza na KIMBUNGA iliyoandikwa na HAJI GORA msanii ametoa ujumbe ufuatao;

Tabaka tawala kuwasikiliza tabaka tawaliwa; Msanii amehamasisha tabaka tawala kuwasikiliza tabaka tawaliwa, na siyo kutoa maamuzi bila kuwashirikisha tabaka tawaliwa. Mfano kwenye shairi la Paka.

Usawa katika jamii; Msanii ameweka mkakati wa usawa katika jamii, yaani kusiwe na matabaka akuyo wengine wanu baki wanateseka na wengine wakifurahi. Kwa mfano katika shairi la Punda, Lupa inaonyesha jinsi tabaka la chini linavyo teseka


Kupinga na kukataa rushwa; Msanii amehamasisha katika kupinga na kukataa rushwa katika jamii. Kwa mfano katika shairi la kimbunga inaonyesha jinsi rushwa ilivyo shika hatima ya serikali na kufanya mambo yakachanganyikana.

Kielelezo Na.13.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5.

### 2.2.2.2 Swali la 6: Uhakiki wa Ushairi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, katika mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kuonesha jinsi lugha ya picha ilivyotumika kubeba ujumbe wa wasanii katika diwani mbili kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na watahiniwa wengi (asilimia 96.4) waliofanya mtihani wa Kiswahili. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 23,344 sawa na asilimia 96.68 walipata alama kuanzia 6.5 hadi 20 kama inavyoonekana katika Chati Na. 10.




Chati **Na. 10**: *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 6*

Katika Chati Na. 10, watahiniwa 802 (3. 32%) walipata alama hafifu 0 hadi 6.5, watahiniwa 1,663 (6.89%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 21,681 (89.79%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi (89.79%) walijibu vizuri swali hili na kupata alama kuanzia alama 12 hadi 20. Watahiniwa walionesha umahiri wa kiwango cha juu ambapo kati yao, asilimia 11.9 walikuwa na ufaulu mzuri zaidi kwani walipata alama 18 hadi 20. Majibu mazuri ya watahiniwa hao yalitokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu namna lugha ya picha inavyotumika kubeba ujumbe wa wasanii katika diwani teule.

Baadhi ya watahiniwa katika kundi hilo waliweza kufafanua kwa usahihi hoja tatu kwa kila diwani wakionesha jinsi lugha ya picha ilivyotumika kubeba ujumbe wa wasanii katika diwani mbili walizosoma. Miongoni mwao walifafanua hoja sahihi kuhusu lugha za picha mbalimbali zilizotumika katika diwani kama vile: *kunguru, kasuku* na *paka shume,* katika diwani ya "Fungate ya Uhuru" na *punda*, *paka* na *kibwangai* kwenye diwani ya "Kimbunga." Watahiniwa hao walifafanua kwa usahihi namna ambavyo picha hizo zimetumika kubeba ujumbe wa wasanii katika diwani teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa ufafanuzi mzuri uliojitosheleza katika diwani ya "Kimbunga" kama vile, *kibwangai* (kiongozi msaliti), *paka* (mtu mdokozi/mwizi) na *punda* (mtu asiye na shukrani). Kutoka kwenye diwani ya "Chungu Tamu" alionesha matumizi ya lugha ya picha zifuatazo: *chatu* (mtawala), *mayai* (malighafi) na *kuku* (mtawaliwa) na kueleza kwa usahihi namna zilivyotumika kubeba ujumbe wa msanii katika diwani husika. Pia, aliandika utangulizi na hitimisho linaloendana na swali na alifafanua vizuri hoja zake kwa mifano sahihi kutoka katika diwani teule. Kielelezo Na.14.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

06 Ujumbe ni mawazo yanayotolewa kati
ka kazi ya fasihi na pia huwa ndani ya vi
pengele vya lugha kama vile methali, Nahau
tusemsa. ~~Kwa~~ Ni kweli kuwa ujumbe wa kazi
ya msanii huwa ndani ya vipengele vya lugha
kwa kutumia diwani ya KIMBUNGA iliyoandi
kwa na HAJI GORA na diwani ya CHUNGU
TAMU iliyoandikwa na THEOBALD A. MVUNGI
zifuatazo ni hoja zinazoonyesha picha lugha ya
picha iliyojitokeza kubeba ujumbe wa wasa
nii katika diwani. Kwa kuanza na diwani ya
KIMBUNGA kama ifuatavyo .

Picha ya kimbwangai; Msanii ametumi
a picha hii kuonyesha au akimaanisha kiongozi
mwalriti kama asemavyo msanii

"Kimbwangai alipoona, ati mtu kakamilika,
Akaanza kujivuna, na dharau kuzidia
Katu hakujali tena, wenzake walimwambia
Akazani umbo lile, nyani hawi tena."

Hivyo kutokana na picha hii tunapata ujumbe
kuwa "Mpanda ngazi hushuka". Ipo siku moja
tu utarudi ulikotoka kama kimbwangai alivyo
rudi kuwa nyani tena.

Picha ya Paka; Msanii ametumia
picha akimaanisha mtu mdokozi. Katika shai
ri la "Paka" msanii anasema.

"Paka nakuhasa wizi, wacha kuiba samaki
Imekuwa yako kazi, majikoni huondoki
Utaleta uchokozi, ishitu kizuri kiki"

Kwa hiyo hapa tunapata ujumbe kuwa "tabi
a ya udokozi haifai katika jamii utakuja
kuumia".

06 Picha ya Punda; msanii ametumia picha hii akimaanisha kuwa punda ni mtu asiye na shukrani, katika shairi la "PUNDA" msanii anasema.

"Punda hakumbuki wema, hata kwa mchunga wake,
Humpa mwingi mtama, na maji asitirike
Katu hawi salama, shukrani yako mateke
Ndiyo tabia ya punda, kutuchakurusha mateke
Kuchunga akikuchinda, Mwache aende zake"

Hivyo kutokana na picha hii tunapata ujumbe kuwa "yatupasa kushukuru kwa kila jambo kwani shukrani ni muhimu".


Pia kwa kutumia diwani ya ~~CHATU~~ ~~na~~ CHUNGU TAMU zifuatazo ni hoja zinazoonyesha jinsi lugha ya picha ilivyotumika kubeba ujumbe wa wasanii katika diwani.

Picha ya chatu; katika hii diwani msanii ametumia picha ya chatu akimaanisha "mtawala". katika shairi la "chatu na kuku" kama asemavyo msanii

"Adha imemkumba
Hasira amesfumbata
mayai akayataga
Japo kwa woga
chatu akayameza
Wakamsifu paku kwa kumbeza"

Kutokana na picha hii tunapata ~~ku~~ujumbe kuwa "tabaka tawala hunyang'anya haki za raia wa chini"

Picha ya mayai; Msanii ametumia mayai ~~ku~~ akimaanisha kuwa ni maliasili. kati




06 Ka shairi la "CHATU na KUKU" Msanii anasema,
"---- Mayai akayatafaga
japo kuwa mwoga
chatu akayameza
Wakamsifu paku kwa kumbeza"
Katika picha hii tunapata ujumbe kuwa "tabaka la tawala huwapora au huwanyang'anya tabaka tawaliwa malighafi zao pasipo ridhaa zao"
Picha ya kuku; Msanii ametumia picha hii kumaanisha kuwa kuku ni mtawaliwa katika shairi la "Chatu na kuku" msanii anasema
"---- Mayai akayatafaga
japo kuwa mwoga
chatu akayameza
Wakamsifu paku kwa kumbeza"
Kutokana na picha hii tunapata ujumbe kuwa "tabaka la chini ni chanzo cha maendeleo kwa tabaka tawala kwani huila nguvu zao"
Kwahiyo ni kweli kwamba ujumbe wa kazi ya msanii huwa ndani ya vipengele vya lugha mfano lugha ya picha. Hivyo basi hatuna budi kuvitumia vizuri vipengele hivi vya lugha ili kufikisha ujumbe unaokusudiwa kwa jamii husika.

Kielelezo Na. 14.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 6.

Katika Kielelezo Na. 14.1, mtahiniwa alielezea kwa usahihi lugha za picha mbalimbali zilizotumiwa na wasanii katika diwani ya “Kimbunga” na “Chungu Tamu” na jinsi zinavyobeba ujumbe kwa jamii waliyokusudia.

Watahiniwa 1,663, sawa na asilimia 6.89, waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5. Ufaulu huo ulichangiwa na sababu mbalimbali. Baadhi ya watahiniwa walibainisha baadhi ya lugha za picha kwa usahihi lakini wakashindwa kutoa ufafanuzi unaojitosheleza katika kueleza namna picha hizo zilivyotumika kubeba ujumbe wa wasanii katika diwani teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika diwani ya “Chungu Tamu” alibaini kwa usahihi picha ya kuku ilivyotumiwa na msanii kama mwizi wa mali ya umma badala ya kumwelezea kuku kama mnyonywaji ambaye ‘chatu’ anamsubiria atage mayai kisha ayafaidi. Katika diwani ya ‘Fungate ya Uhuru’ Mtahiniwa mwingine alitumia lugha ya picha ya *paka shume* kuwa ni mdokozi na mtu mwenye tamaa ya uongozi*; Mjamzito* inawakilisha viongozi waoga na *fungate* inawakilisha ulimbwende wa viongozi; majibu yasiyojitosheleza Hali kadhalika, watahiniwa wa kundi hili walishindwa kutumia mifano ya mashairi yenye kutumia lugha ya picha kwa usahihi, hivyo kuwa na upungufu katika majibu yao na kupata alama za wastani.

Vilevile, watahiniwa wengine 802, sawa na asilimia 3.32, walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5. Watahiniwa hao walishindwa kuonesha jinsi lugha ya picha ilivyotumika kubeba ujumbe wa wasanii katika diwani teule. Baadhi ya watahiniwa walijadili dhamira mbalimbali katika diwani hizo kama vile, *kujitoa mhanga, kupinga suala la matabaka na ubaguzi wa rangi na kupinga uongozi mbaya* (Chungu Tamu) kinyume na matakwa ya swali. Wengine walieleza vipengele vya fani katika ushairi, kama vile; *muundo, mtindo, wahusika* na *mandhari* badala ya kubainisha picha/taswira mbalimbali zilivyotumika kubeba ujumbe wa wasanii katika diwani teule, hivyo kupata alama hafifu. Kielelezo Na.14.2 kinaonesha sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili.



6 "Ujumbe wa kazi ya msanii huwa ndani ya vipengele vya lugha" Kwa kutumia diwani ya "Mapenzi bora" iliyoandikwa na Shabani Robert na diwani ya "Fungate ya Uhuru" tunaweza kuona ni kwa namna gani ujumbe huwa ndani ya vipengele vya lugha kama ifuatavyo:-

Taswira:- Katika diwani ya "Fungate ya Uhuru" kipengele cha taswira mwandishi ametumia hususani mwandishi alivyoandika shairi la "Njiwa wangu" akiwa ana maanisha Msichana hivyo njiwa ametumika kama msichana. Pia katumia neno Papa akimaanisha watu wenye pesa na ambao wanajiona.

Tamathali za semi:- Katika diwani ya "Mapenzi bora" mwandishi ameweza kufikisha ujumbe kwa kutumia Vipengere vya lugha. Mwandishi alitumia sitiari, Tashtiti, Tashibiha katika mashairi yake ambapo kutokana na matumizi hayo lengo au ujumbe ulifikika vizuri.

Muundo:- Katika diwani ya "Mapenzi Bora" mwandishi ametumia muundo wa moja kwa moja katika masimulizi yake na pia ametumia muundo wa mistari nane na mine.

Mtindo; Katika diwani ya "Mapenzi bora" mwandishi ametumia mtindo wa kimapokeo kwani kumekuwa na urari wa vina katika beti zote za mashairi yake.


Kielelezo Na.14.2: Sampuli ya sehemu ya jibu lisilo sahihi ya swali la 6.

Katika Kielelezo Na.14.2, mtahiniwa alifafanua kimakosa vipengele vinavyotumiwa na wasanii kama vile *taswira, tamathali za semi, muundo, mtindo* na *madhari* ili kubeba ujumbe kwa jamii ambapo hakutumia mifano yoyote kutoka katika diwani teule, hivyo kupata alama hafifu.

#### 2.2.2.3 Swali la 7: Uhakiki wa Riwaya

Takwimu zinaonesha kuwa katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *Uhakiki wa Riwaya*. Swali lililenga kupima uwezo wa kutathmini na lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kauli kuwa harakati za kutafuta maendeleo na haki hukwamishwa na watu wenyewe ndani ya jamii kwa kutoa hoja tatu kutoka katika kila moja kati ya riwaya mbili alizosoma.

Watahiniwa 24,151 sawa na asilimia 96.8 walijibu swali hili. Swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri zaidi kwa sababu watahiniwa 24,131, sawa na asilimia 99.51 walipata alama kuanzia 6.5 hadi 20. Chati Na.11 inaonesha viwango vya ufaulu kwa watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na.11:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Katika Chati Na. 11, watahiniwa 120 (0. 49%) walipata alama hafifu 0 hadi 6.5, watahiniwa 909 (3.75%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 23,222 (95.76%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Jumla ya watahiniwa 23,222 sawa na asilimia 95.76 walifanya vizuri swali hili na kupata alama kuanzia 12 hadi 20. Ufaulu mzuri katika swali hili ulitokana na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Uhakiki wa Riwaya*. Baadhi ya watahiniwa waliweza kuthibitisha kauli isemayo kuwa ''Harakati za kutafuta maendeleo na haki hukwamishwa na watu wenyewe ndani ya jamii'' kwa kutoa hoja tatu kutoka katika kila riwaya mbili walizosoma. Kwa mfano, katika riwaya ya "Kufikirika" watahiniwa walionesha namna Mfalme


alivyothamini imani ya makafara ya damu na matambiko hatimaye kukwamisha maendeleo ya jamii ya Kusadikika. Aidha, katika riwaya ya "Mfadhili" watahiniwa walionesha namna wahusika *Dania na Gaddi* walivyokwamisha maendeleo katika jamii kutokana na suala la mapenzi wakiwa kazini. Vilevile, katika riwaya ya "Vuta N'kuvute walithibitisha kauli hiyo kwa kutumia mhusika Koplo Matata alivyokwamisha harakati za maendeleo kwa kuwasaliti wenzake akina, Denge, Mambo, Chande na Mwajuma na kujiunga na wakoloni (Inspecta Wright). Mtahiniwa mmoja alithibitisha kwa usahihi kauli hiyo kwa kuonesha namna wahusika kama *Dania na Jerry alivyoleta migogoro katika ndoa hatimaye kuathiri utendaji wa kazi zao* kutoka katika riwaya ya "Mfadhili." Vilevile *Shihab na wazazi wa Yasimin* waliwatweza wanawake katika "Vuta Nkuvute" na kukwamisha maendeleo yao katika harakati za kutafuta haki katika jamii. Kielelezo Na.15.1 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

07. Ni kweli harakati za kutafuta maendeleo na haki, hukwamishwa na watu wenyewe ndani ya jamii". Kwa kutumia riwaya ya "MFADHILI" iliyoandikwa na Hussein Tuwa na riwaya ya "VUTA N'KUVUTE" iliyoandikwa na Shafi Adamu Shafi. Kwa kuanza na riwaya ya "MFADHILI" jinsi harakati za kutafuta maendeleo na haki zilivyo kwamishwa na watu wenyewe ndani ya jamii kama ifuatavyo:

Dania, huyu ni muhusika ambaye anakwamisha maendeleo katika jamii kwa kujiingiza katika ~~ule~~ ulevi wa kupindukia mwisho anashindwa kuendelea na kazi kutokana na uzembe wake katika kazi, hivyo anapewa likizo na Mama Mlolo ili akapumzike, kutokana na Dania kupewa likizo kile ngo chake kinabaki bila mtu. Hivyo basi maendeleo ya jamii yanaendelea kudumaa

Jelly, huyu pia ni muhusika aliyechangia kukwamisha maendeleo katika jamii kipindi anamsaliti Dania na kuamua kumbia wakati Dania anaumwa badala ya kumsaidia lakini Jelly anakimbia, watu kama Jelly wanaokimbia matatizo badala ya kuyasuluhisha ni kikwazo cha maendeleo katika jamii.

Nyambuja, muhusika huyu ni kikwazo cha maendeleo kwasababu kutokana na usaliti wake kwa Gaddy kunapelekea Gaddy kujiingiza katika ulevi kwasababu ya mawazo aliyo kuwa nayo na hatimaye Gaddi anasaini Nyaraka za uongo katika kampuni yake, hivyo


07 Serikali inapata hasara ambapo hupelekea kukwama kwa maendeleo ya jamii. Hivyo walifi ni kikwazo cha maendeleo

Kwa kumalizia na riwaya ya "VUTA N'KUVUTE" jinsi watu wanavyokwamisha harakati za kutafuta maendeleo na haki katika jamii kama ifuatavyo:

Shibab, huyu ni muhusika aliyecha ngia kukwamisha kwa maendeleo kwasababu alimuweka Yasmini utawani, hivyo Yasmini alishindwa kufanya kazi ili alete maendeleo katika jamii lakini kwa Yasmini ilikua ndani na Yasmini, Yasmini na ndani, hii yote ni kutokana na wivu wa Shihab kwa mke wake Yasmini.

Wazazi wa Yasmini, hawa pia ni kikwazo kikubwa cha maendeleo katika jamii kwasababu wanamlazimisha Yasmini kuolewa na mzee asiyempenda, hivyo Yasmini anakosa uhuru wa kufanya mambo ya maendeleo kwa ajili ya Bwana Raza, lakini hata maye Yasmini anafanikiwa kumtoroka Bwana Raza. Hivyo wazazi wasikilize mahitaji ya watoto wao ili kuleta maendeleo ya jamii.

Kopolo Matata, huyu ni muhusika ambaye ni mwafrika lakini anasaidiana na wazungu kuhakikisha waafrika hawapati uhuru wao. Mfano Kopolo Matata anawakamata watu wanaopigana ili kupata uhuru wa nchi yao. Kama vile Denge na kundi lake hata hivyo Denge na rafiki zake wanashindwa kutokana na ujinga wa Kopolo matata

Kielelezo Na.15.1: Sampuli ya sehemu ya jibu sahihi katika swali la 7.


Katika Kielelezo Na. 15.1, mtahiniwa alithibitisha kauli kuwa harakati za kutafuta maendeleo na haki hukwamishwa na watu wenyewe ndani ya jamii. Mtahiniwa alitoa hoja sahihi katika riwaya ya “Mfadhili” na “Vuta N’kuvute” japokuwa alikuwa na tatizo la kitahajia katika kazi yake lakini aliweza kupata alama za juu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 909 sawa na asilimia 3.75 walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5. Ufaulu wa wastani wa watahiniwa katika kundi hilo ulitokana na sababu tofauti tofauti. Baadhi yao walitoa hoja pungufu japo walizielezea vizuri au kutokuandika utangulizi na hitimisho katika kazi zao. Wengine walitoa hoja zisizojitosheleza katika kuthibitisha kauli kuwa, *harakati za kutafuta maendeleo na haki hukwamishwa na watu wenyewe ndani ya jamii*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea wasifu wa ndani na wa nje wa wahusika kama vile; ‘Mfadhili’ (*Gadi Bullah*, *Dania* na *Jerry* na *Denge*, *Yasmin* na *Mwajuma* (Vuta N’kuvute) lakini alishindwa kuthibitisha kwa mifano sahihi kutoka katika riwaya hizo, hivyo walipata alama za wastani.

Hali kadhalika, watahiniwa 120, sawa asilimia 0.49 walishindwa kujibu kwa usahihi swali lililowataka kuthibitisha kuwa, *harakati za kutafuta maendeleo na haki hukwamishwa na watu wenyewe ndani ya jamii’’* kwa kutoa hoja zisizojitosheleza, hivyo kupata alama hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5. Kutokana na kukosa umahiri katika uhakiki wa riwaya, baadhi ya watahiniwa walibainisha wahusika katika riwaya teule na kueleza namna wanavyofaa kuigwa na kutoigwa kinyume kabisa na matakwa ya swali. Wengine walijadili wahusika katika tamthiliya teule badala ya riwaya teule kama swali lilivyohitaji. Kwa mfano; *Aisha na Nungunungu*, *Jalia na Mlemeta* na *Nungunungu* ni wahusika wa tamthiliya ya Morani, lakini mtahiniwa huyo ameonesha kuwa ni wahusika wa riwaya ya ‘Vuta N’kuvute. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijadili dhamira zilizojitokeza katika riwaya teule kama vile; uvivu, wizi, ulevi katika tamthiliya ya “Mama N’tilie” kinyume na matakwa ya swali. ‘Kwa ujumla watahiniwa walitakiwa kuthibitisha kauli kuwa, ‘*harakati za kutafuta maendeleo na haki hukwamishwa na watu wenyewe ndani ya jamii* kwa kuelezea namna wahusika katika riwaya hizo walivyojikwamishia maendeleo yao

wenyewe. Kielelezo Na.15.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kinyume na matakwa ya swali.

01 Maendeleo Ni kitendo cha mtu au watu
au taifa kutoka hali ya chini na kwenda hali
ya juu. Maendeleo yanaweza kuwa niya kisiasa,
kiuchumi na kiutamaduni na hata kijamii katika
hali hii ya kutaka maendeleo kuna watu huwa
wanaleta vikwazo au vipingamizi katika kufanikisha
lengo kwa kutumia tamthiliya ya MORANI iliyoandi
kwa na EMMANUEL MBOGO na Tamthiliya ya NGUZO-
MAMA iliyoandikwa na PENINA MUHANDO kuonesha
jinsi msanii alivyoonesha watu wanavyoweza kukwa
misha maendeleo ya jamii kwa kuanzia Tamthiliya
ya MORANI zifuatazo ni hoja ambazo watu -
hutumia kukwamisha maendeleo kama ifuatavyo.
Uhujumu Uchumi; hiki ni kitendo cha
mtu kutumia mali ya umma kwa maslai yake -
binafsi katika tamthiliya hii mwandishi anemtu
mia mhusika Nunqununqu ambaye alikuwa ana
tumia mali ovyo za serikali kwa maslai yake
mfano katika ukurasa wa 46? Jario: anaposema
" Unajua nunqununqu anavusha kabawana
karafuu kwenda nchi jirani kwa magendo "
Husemi mlemeta! Unajua ana hoteli kubwa
marekani na benki uko Uswisi
kwaiyo katika jamii kuna watu kama Nunqununqu -
ambao wanahujumu uchumi wa nchi
Uzurufu; Ni kitendo cha mtu mzima ku-
fanya mapenzi na mtoto hapo msanii anamuonesha -



7 NunguNungu ambaye anapenda mapenzi na mtoto wa shule ambaye ni Aisha kwa sababu anamsababisha hadi Aisha anafukuzwa shule kwa sababu ya mapenzi kwenda anaposoma angeleta maendeleo makubwa (UK 26) anaposema Aisha

"mpumbavu, mpumbavu? mimi mpumbavu tuliku wa tukiwa kesho bao hadi usiku wa manane leo – Unasema mpumbavu, umenisababisha hadi nafukuzwa shule

katika jamii kuna watu kama NunguNungu ambao wanatumia ovyo uzee wao kwa kutoka na watoto.

Usaliti, Ni kitendo cha mtu kwenda kinyume na mawazo ya wenzake mwandishi anawatumia wahusika Mlemeta na Yusuph ambao walikuwa wasaliti wa serikali kwa kuficha maovu ya kiongozi mbaya Nungunungu anaposema jasho.

kama mlemeta umenunuliwa sio mimi (UK 23)

katika jamii kuna watu kama Mlemeta ambao huwasaliti wenzao kwa kuletea uovu

kwa kumalizia tamthiliya ya Nguzo mama inaonesha kwa vipi watu hukwamisha maendeleo ya jamii yao, kama ipuatavyo.

Uongozi mbaya; Ni hali ya kiongozi kutowajibika ipasavyo katika kazi yake mfano – anamtumia mhusika Bi nne ambaye aliandika mashtaka ya uongo kuhusu Bi Nane kwa lengo la kumgandamiza mwenzake katika (UK 22-23) anaposema " walimu wenzake wanamchukia kwa tabia yake mbaya"

katika jamii kuna watu kama Bi nne ambao wana kwamisha maendeleo.


Kielelezo Na. 15.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo Na.15.2 mtahiniwa, alieleza dhamira mbalimbali katika tamthiliya ya *Nguzo Mama* na *Morani* kama vile, *uongozi mbaya, usaliti, uvivu, uhujumu uchumi, uzurufu na usaliti* kinyume kabisa na matakwa ya swali.

### 2.2.2.4 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, katika mada ndogo ya *Uhakiki wa Tamthiliya*. Swali lilimtaka mtahiniwa kutathmini umuhimu wa matumizi ya nyimbo na masimulizi katika tamthiliya mbili alizozosoma kwa kutoa hoja nne kwa kila kitabu.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,645 sawa na asilimia 6.6 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu. Kati yao, watahiniwa 1,383 sawa na asilimia 87.7, walifaulu vizuri kwani walipata alama kuanzia 7 hadi 19. Chati Na.12 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 16.




**Chati Na.12**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Katika Chati Na. 12, watahiniwa 262 (15. 93%) walipata alama hafifu 0 hadi 6.5, watahiniwa 604 (36.72%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 779 (47.36%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 19.

Kulingana na takwimu, watahiniwa 779 sawa na asilimia 47.4 walikuwa na ufaulu mzuri kwani walipata alama kuanzia 12 hadi 19. Miongoni mwao, watahiniwa 48, sawa na asilimia 2.9 walifaulu vizuri zaidi na kupata alama za juu kuanzia 18 hadi 19. Kwa ujumla watahiniwa katika kundi hili waliweza kutoa hoja sahihi za kutathmini

umuhimu wa matumizi ya nyimbo na masimulizi katika tamthiliya mbili walizosoma. Kwa mfano, Katika tamthiliya ya "Morani" watahiniwa walielezea umuhimu wa matumizi ya *nyimbo* katika *huhifadhi amali za jamii*, *huelimisha/hufunza jamii* na *huburudisha*. Pia walionesha umuhimu wa matumizi ya masimulizi kama vile *kukuza lugha* na *kuelimisha.* Vilevile walionesha namna nyimbo zinavyoleta uhai wa tamthiliya na kumpa pumzi msomaji anapoimba. Aidha, matumizi ya nyimbo hupamba kazi ya tamthiliya na kuishirikisha hadhira ipasavyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu swali hili vizuri kwa kuandika utangulizi mzuri na hitimisho zuri pamoja na kutathmini umuhimu wa matumizi ya nyimbo na masimulizi katika tamthiliya teule kama Kielelezo Na.16.1 kinavyoonesha sehemu ya jibu la mtahiniwa huyo aliyejibu vizuri swali hili.

08. Matumizi ya nyimbo, ni mtindo ambao unatumika katika kazi ya kifasihi ambapo humtofa utiiha mtanii mmoja na mwingine pia.

Masimulizi, ni hali ya kuelezea kitu ambapo hali hii hufanywa na fanani mwenyewe. Ni kweli kwamba kuna umuhimu wa matumizi ya nyimbo na masimulizi katika tamthiliya, kwa kutumia tamthiliya kwa kuanza na tamthiliya ya "Kivuli kinaishi" na Nguzo MAMA kilichoandikwa na "Penina mhando".


Kwa kuanza na tamthiliya ya "NGUZO MAMA" kilichoandikwa na "Penina mhando" tunaona jinsi ambavyo Matumizi ya nyimbo na masimulizi ni muhimu sana.

Hivyo ~~kazi ya~~ wasomaji fasihi, Hapa tunaona jinsi ambavyo kamanda wa patata walivyokuwa wakiimba na tunaona jinsi ambavyo kazi hiyo inaonekana kuwa bora na nzuri. mwandishi anaonesha jinsi walivyokuwa wanaimba

Tukupambeje Mama X 2

Tukupambeje Mama X 2

Hivyo kutokana na uwepo huo wa nyimbo tunaona jinsi wasomaji wa kazi ya fasihi wanavutika na kuamua kusoma kwa ubora na uzuri wa fasihi yake hivyo kutokana na hali hiyo tunaona jinsi ambavyo hali hii inapelekea uwepo kwa wasomaji wengi.



08. Matumizi ya nyimbo, Huondoa uchovu kwa kusoma; Hivyo mtu anapokuwa anasoma au anaona kati kukiimba inakuwa inampunguzia yeye mwenyewe uchovu hivyo hali hiyo inaweza kupelekea hata kazi husika kusoma au kuangalia bila kuchoka. mfano kanawake kupotelea wanavyoimba "Tukupambeje Mama x2" inaleta umakini wa kusikiliza.

Matumizi ya masimulizi; Husaidia kuonesha mandhari halisi Hapa tunaona mtu anapoanza kusimulia anaonesha hali halisi ambayo ipo katika eneo husika hivyo hutufanya tuwe waelewa na eneo au Mahali husika. Mwandishi katika kazi yake anaonesha R: Msimulizi anapoanza,
R: Msimulizi! Hadithi hadithi
kusikiliza! Hadithi njoo
Hivyo hufanya jisi kujua mandhari ya mwanzo.

Matumizi ya masimulizi pia, Husaidia kuondoa uchovu, kwani huwasha utendaji kwa kuongea, kupiga makofi kwa hiyo kutokana na uwepo wa hali hiyo tunaona jinsi ambavyo matumizi haya humfanya hadhira kuelewa na kufanya kazi husika kwa uhoru wa aina yake.

Kielelezo Na. 16.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 8.

Aidha, watahiniwa 604 sawa na asilimia 36.7 walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa matumizi ya nyimbo na masimulizi katika tamthiliya teule. Kutokana na kukosa weledi huo, baadhi ya watahiniwa waliandika utangulizi na hitimisho lisiloendana na swali. Pia walijadili hoja bila kutumia mifano dhahiri ya matumizi ya nyimbo na masimulizi kutoka katika tamthiliya teule.

Watahiniwa wengine walionesha namna nyimbo zinavyojitokeza katika tamthiliya teule bila kuelezea umuhimu wake, hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa 262, sawa na asilimia 15.9 waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kuwa na uelewa mdogo kuhusu umuhimu wa matumizi ya nyimbo na masimulizi katika tamthiliya. Baadhi ya watahiniwa walitoa hoja zisizo sahihi katika kuonesha umuhimu wa matumizi ya nyimbo na masimulizi katika tamthiliya. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zifuatazo katika tamthiliya ya ‘Morani: *huchochea ushirikiano, huchochea maendeleo na ujasiri, hukosoa jamii, huelimisha jamii* na katika tamthiliya ya ‘Nguzo Mama alitoa hoja kama vile *husaidia kuchochea maendeleo, kuelimisha jamii, kujenga ushirikiano na kuburudisha jamii*; hoja ambazo zilikuwa kinyume kabisa na matakwa ya swali. Watahiniwa wengine walijadili dhamira mbalimbali katika tamthiliya teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika tamthiliya ya “Kivuli Kinaishi” alitoa hoja kama; *rushwa, matabaka* na *imani za kishirikina* na katika tamthiliya ya “Kwenye Ukingo wa Thim”; alibainisha *kimakosa mila potofu katika jamii, malezi mabaya, na uongozi mbaya*, hivyo kupata alama za chini. Kielelezo Na.16.2 ni sampuli ya sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

8 Matumizi ya nyimbo na masimulizi
katika tamthiliya ni mbinu inayotumika
kufikisha ujumbe kwa jamii, kwa
kutumia tamthiliya mbili ambazo ni
"Kivuli kinaishi" iliyo andikwa na "Said
Mohamed" na "Kwenye ukingo wa Thim"
iliyo andikwa na "Ebrahim Husseni"
Ifuatao ni umuhimu wa matumizi
ya nyimbo na masimulizi. katika
tamthiliya hizo kama zilivyo jadiliwa
na waandishi
Kwa kuanza na Tamthiliya
ya "Kivuli Kinaishi" mwandishi ameo-
nesha umuhimu wa nyimbo na
masimulizi kama ifuatavyo.
Kuonesha rushwa katika
jamii, mwandishi ameonesha hili kwa
kumtumia muhusika mtolewa baada
ya kupatazwa na bawabu [illegible] kuingia
katika jamii ya Giningi hivyo kubaini-
mika kutoa rushwa ya shilingi 5000/=
ndipo akaruhusiwa
hivyo [illegible] kuonesha matabaka katika
jamii kwani tunaona masimulizi ya
Bi kizee ndiyo yaliyo ibua hili jambo
Kuonesha matabaka Katika
jamii, Mwandishi anamuonesha Bi. kirembwe
aliyo kuwa tawala dikteta
aliyekuwa anatawala kwa mabavu
pia kulikuwepo na watawaliwa
kama mtolewa na wali kai ambao
walikuwa wananyanyasika na mfumo

Kielelezo Na.16.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 16.2, mtahiniwa alieleza kuwa matumizi ya nyimbo na masimulizi katika tamthiliya hulenga kuonesha dhamira mbalimbali kama vile *matabaka, rushwa* na nyinginezo kinyume na matakwa ya swali.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa somo la Kiswahili unaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri katika mada tisa (9) na ufaulu wa wastani katika mada mbili (2).

Ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2022 umeongezeka katika mada nne ikilinganishwa na mwaka 2021. Mada hizo ni: Utungaji (99.92%), Utumizi wa Lugha (97.96), Maendeleo ya Kiswahili (98.72%) na Ushairi (98.19%). Ongezeko la ufaulu katika mada hizo ulikuwa wa asilimia 1.82, 7.86, 1.32 na 14.79, mtawalia. Ongezeko la ufaulu katika mada ya *Ushairi* linaonesha kuwa jitihada kubwa zimefanyika katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada hii iliyokuwa na historia ya ufaulu wa chini kwa miaka iliyotangulia.

Kwa upande mwingine, ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2022 umepungua katika mada saba (7) ikilinganishwa na mwaka 2021. Mada hizo ni : Riwaya (99.51%), Ufahamu na Ufupisho (94.69%), Fasihi kwa Ujumla (87.30%), Tamthiliya (84.07%), Matumizi ya Sarufi (61.43%), Usanifu wa Maandishi (53.55%) na Tafsiri na Ukalimani (44.08%). Kushuka kwa ufaulu kulitofautiana kati ya mada moja na nyingine ikilinganishwa na ufaulu wa mada hizo kwa mwaka 2021. Mada za *Riwaya*, *Fasihi kwa Ujumla* na *Ufahamu na Ufupisho* zilikuwa na muachano mdogo wa asilimia 0.29, 4.81 na 3.2 mtawalia. Aidha, mada za *Tamthiliya*, *Matumizi ya Sarufi*, *Usanifu wa Maandishi* na *Tafsiri na Ukalimani* zilikuwa na muachano mkubwa wa asilimia 10.33, 21.67, 30.85 na 52.82 mtawalia. Mada za *Usanifu wa Maandishi* (*53.55*%) na *Tafsiri na Ukalimani* (*44.08*%) zilikuwa na ufaulu wa wastani na zilionekana kuwa na muachano mkubwa zaidi wa ufaulu ikilinganishwa na ufaulu wa mada hizo kwa mwaka 2021.

Licha ya kushuka kwa ufaulu katika baadhi ya mada, kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika mada zote kwa mwaka 2022 ulikuwa mzuri sawa na mwaka 2021 ambapo, asilimia 100 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 35 katika mada zote. Hii inatokana na sababu zifuatazo: uelewa wa kutosha kuhusu mada nyingi zilizotahiniwa, matumizi sahihi ya lugha na uzingatiaji wa alama za uandishi, matakwa ya swali na kutoa hoja sahihi zenye mifano thabiti.

## 4.0 HITIMISHO

Taarifa hii inaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika mtihani wa 121 Kiswahili kwa mwaka 2022 kilikuwa kizuri kwani asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu. Jumla ya mada tisa (9) zilikuwa na ufaulu mzuri na mada mbili (2) zilikuwa na ufaulu wa wastani. Kiwango hiki cha ufaulu wa watahiniwa kwa ujumla kimefanana na kiwango cha ufaulu cha mwaka 2021, ambapo watahiniwa wote waliofanya mtihani huo walifaulu.

Uchambuzi uliofanyika unaonesha kuwa, watahiniwa walifanya vizuri mtihani wa somo hili la Kiswahili kutokana na sababu kama vile: kujibu kulingana na mahitaji ya swali, uelewa mkubwa wa mada kuu na mada ndogo, uwezo mkubwa katika kujibu maswali na kutetea hoja kwa kutumia mifano. Hata hivyo mada za *Usanifu wa Maandishi* na *Tafsiri na Ukalimani* zilikuwa na ufaulu wa wastani kutokana na kuwa na majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ufaulu wa somo la Kiswahili ni mzuri kutokana na juhudi kubwa zinazofanywa na serikali na wadau wengine wa elimu. Hata hivyo, ili kuinua kiwango cha ufaulu katika mada zilizokuwa na ufaulu wa wastani, yafuatayo yanashauriwa kufanyika:

(a) Walimu watumie njia za Midahalo kuwaongoza wanafunzi wasome matini mbalimbali za kifasihi kwa ajili ya kubaini mbinu mbalimbali za kisanaa zilizotumika katika matini hizo ili kujiongezea umahiri katika kusanifu maandishi.

(b) Walimu wawaongoze wanafunzi kufanya mazoezi ya kutafsiri matini katika mikabala ya kimawasiliano na kisemantiki na kuwapa mrejesho kwa wakati ili kuwapa ujuzi wa kutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika miktadha mbalimbali.

(c) Walimu wawaongoze wanafunzi kufanya mazungumzo yenye tija ili kupata umahiri wa kutumia sarufi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa ufasaha.

(d) Walimu wawahimize wanafunzi kusoma vitabu vya kiada na ziada na majarida/machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada zote ili wawe wabobezi zaidi katika mada mbalimbali.

*Kiambatisho A*

## UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2022

| Na. | Mada | Idadi ya maswali | Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa kwa Swali | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | *Utungaji* | 1 | 99.92 | Vizuri |
| 2. | *Riwaya* | 1 | 99.51 | Vizuri |
| 3. | *Maendeleo ya Lugha* | 2 | 98.72 | Vizuri |
| 4. | *Ushairi* | 2 | 98.19 | Vizuri |
| 5. | *Utumizi wa Lugha* | 1 | 97.96 | Vizuri |
| 6. | *Ufahamu na Ufupisho* | 1 | 94.69 | Vizuri |
| 7. | *Fasihi kwa Ujumla* | 3 | 87.30 | Vizuri |
| 8. | *Tamthiliya* | 1 | 84.7 | Vizuri |
| 9. | *Matumizi ya Sarufi* | 1 | 61.43 | Vizuri |
| 10. | *Usanifu wa Maandishi* | 1 | 53.55 | Wastani |
| 11. | *Tafsiri na Ukalimani* | 1 | 44.08 | Wastani |

*Kiambatisho B*

**ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MWAKA 2021 NA 2022**

